Alhamisi Januari 25, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581566

MWANGA WA JAMII

LIKE & FOLLOW US
www.twitter.com/nipashetz
www.ippmedia.com
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper



**GHANA YAONDOLEWA, YAMTIMUA HUGHTON**

UKURASA 21

# HISTORIA

• **Maandamano** CHADEMA yafanyika kwa amani, wawasilisha ujumbe UN, polisi wawalinda... *Endelea ukurasa 2*



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Taifa, Freeman Mbowe, Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Tundu Lissu na Katibu Mkuu, John Mnyika wakiongoza maandamano ya amani na kuyahitimisha katika Ofisi za Umoja wa Mataifa (UN) Sinza, Dar es Salaam jana. Picha nyingine ni baadhi ya wafuasi wa chama hicho, wakishiriki maandamano hayo. **Picha zaidi Uk. 9. PICHA: IMANI NATHANIEL/MIRAJI**

**MICHEZO** **SIMBA, YANGA SC MAPINDUZI** UK.24 **KATUNI** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan akiwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Soekarno-Hatta, Tangerang kwa ajili ya ziara ya Kitaifa nchini Indonesia jana. **PICHA: IKULU**

# Historia yawekwa siasa za Tanzania

**Na Waandishi Wetu**

NI historia. Ndivyo inavyoonekana baada ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kufanya maandamano ya amani kutoka maeneo mbalimbali Dar es Salaam hadi Ofisi za Umoja wa Mataifa (UN).

Wanachama na wafuasi wa chama hicho walikusanyika katika ofisi hizo wakiwa na mabango ya kutaka maoni ya wananchi kuzingatiwa kwenye mabadiliko ya sheria za uchaguzi, Katiba Mpya na kupanda kwa gharama za maisha.

Maandamano hayo, yakiwa ya kwanza kufanywa na chama cha upinzani huku polisi wakiwalinda, wakiongozwa na Kamanda wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro hadi mwisho wa maandamano hayo, hayajawahi kufanyika. Kila walipoandamana, walikumbana na vipigo kutoka kwa polisi wenye silaha huku wengine wakipoteza maisha.

Hali hiyo imefanya maandamano hayo kuwa historia katika siasa za Tanzania tangu kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi. Hatua hiyo pia imempa sifa Rais Samia Suluhu Hassan ambaye tangu aingie madarakani mwaka 2021, ameonyesha hataki mivutano kisiasa.

Katika kuonyesha hilo pia, Rais Samia alianzisha mazungumzo na vyama vya upinzani na kuwaleta pamoja kwenye mikutano mbalimbali, ikiwamo kuhudhuria Mkutano wa Baraza la Wanawake wa CHADEMA (BAWACHA) huku akija na R4 ambazo ni Maridhiano, Ustahimilivu, Mageuzi na Kujenga upya taifa.

Katika mazungumzo ya vyama vya siasa, CHADEMA haikuhudhuria lakini baadaye yalianzishwa maridhiano ambayo mazungumzo yaliendelea kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM), kukutana na viongozi wa juu wa CHADEMA, ambayo yalibadilisha msimamo wa chama hicho na kuanza kuhudhuria vikao mbalimbali.

Jana, polisi walionekana wakiwa watulivu wakilinda waandamanaji ambao walikuwa na mabango yenye ujumbe mbalimbali kama vile "kikokotoo cha mafao kuondolewa kwa polisi".

Maandamano hayo yalianza saa 3:00 asubuhi katika eneo la Buguruni yakiongozwa na Freeman Mbowe ambaye aliambatana na watoto wake wanne, Mbezi Malamba Mawili wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA Bara, Tundu Lissu aliyesafiri kutoka Afrika Magharibi na kuwasili asubuhi.

Viongozi wa chama hicho walifika ofisi za UN na kuzungumza na viongozi husika, waliotoka nje na kutoa hotuba mbalimbali kwa waandamanaji.

**MULIRO**

Akizungumza baada ya kufanya kikao kifupi cha ndani na Mbowe na Lissu, Muliro, aliwataka wanasiasa kuchunga ndimi zao.

"Yaliyokuwa yakileta msuguano kati ya wasimamizi wa sheria ni aina ya kauli za awali zilizokuwa zikitolewa na baadhi ya viongozi wa vyama, haiwezekani polisi akakaa kimya asijiandae kwa mtu kutangaza wiki kabla kwamba damu itamwagika.

"Itakuwa polisi mjinga wa ajabu mtu anasisitiza kauli hiyo halafu unakwenda unamuangalia kama vile ni mwanachama wa SACCOS ya Kitunda. Polisi hawezi kukuruhusu utembee hata hatua mbili.

"Haya ni mabadiliko makubwa hata kwa wao (CHADEMA) walikuwa wakisisitiza amani, tena mara kadhaa. Tumewaita tumepima akili na kauli zao na wanavyotamka. Nafikiri ni hatua nzuri na muhimu, warekebishe kauli zao turekebishe vitendo vyetu," alisema.

Muliro alisema hata CHADEMA walishangaa kwamba wako naye karibu na kwamba hata wasimamizi wa sheria walikuwa wanashangaa namna polisi walivyokuwa karibu nao wanawaangalia.

"Kimsingi kuna mambo tulisisitiza. Hata kwenye barua yetu tulisema ikitokea uporaji au jambo lolote ambalo ni kinyume cha sheria, tutachukua hatua pale pale kuonyesha nafasi ya jeshi la polisi kikatiba, kisheria na majukumu yake. Kuwepo kwetu hapa ni kuendelea kuwapo kwenye serikali iliyoko madarakani ambayo ni serikali ya watu, kuhakikisha hakuna sheria inayovunjwa kwenye maandamano ya amani," alisema Muliro.

Alisema polisi wamefuatilia kwa karibu kuhakikisha haki moja inayoliliwa na kundi moja haivunji haki ya kundi lingine na kwamba kuwapo kwa maandamano kusizuie watumiaji wengine wa Barabara.

**KAULI YA MBOWE**

Akizungumza baada ya kufika ofisi za UN Tanzania, Mbowe alisema wamefikisha barua rasmi kwa Mwakilishi wa Katibu Mkuu wa UN ambaye ataifikisha kwake na kwamba baada ya kupokewa New York, Marekani itasambazwa kwa umma.

Alisema barua imebeba ujumbe wa waliyokuwa wakizungumza kwenye mikutano na waandishi wa habari, kwenye mabango yao ambayo ni serikali ya CCM kutokutaka kusikiliza maoni ya wananchi kuboresha mifumo ya uchaguzi, kupata Katiba na kupanda kwa gharama za maisha.

"Tumefanya maandamano makubwa na marefu bila sisimizi kuumizwa. Hiyo ndiyo tabia ya CHADEMA. Pale polisi wanapoelewa hoja zetu tunakuwa hatuna ugomvi na mtu yeyote. tutaendelea kuandamana katika taratibu na mikoa mbalimbali hadi wenzetu watuelewe tunaamanisha nini. Kila dirisha linalofaa kugongwa litapigwa ili sauti na kilio cha Watanzania kuhusu mabadiliko chanya kikasikike," alisema

Lissu alisema hoja kwamba inatakiwa tume huru ya uchaguzi na katiba mpya kwa nchi hazikutoka CHADEMA au chama chochote cha upinzani kwa sababu havikuwepo bali yalizungumzwa na Tume Rais ya mfumo wa chama kimoja au mfumo wa vyama vingi vya siasa, maarufu kama Tume ya Jaji Nyalali.

"Tume ya Nyalali ndiyo iliyosema mwaka 1991 kwamba Tanzania inahitaji Katiba mpya na mfumo mpya wa uchaguzi utakaokidhi matakwa ya mfumo wa vyama vingi. miaka 33 leo, bado CCM inatuambia haidhani tunahitaji Katiba mpya au mfumo mpya wa uchaguzi. Tumebembeleza kwa miaka 30, tumeomba kwa miaka 30, sasa tutadai barabarani na hii tumeanza," alisema.

**RC CHALAMILA**

Kabla ya kuanza maandamano, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, aliwatembelea waandamanaji eneo la Mbezi na kuwataka kudumisha amani huku akisema mpango wa kufanya usafi hauhusiani na maandamano hayo.

Kiongozi huyo alitangaza mpango wa kufanya usafi kwa siku ya juzi na jana kwa kushirikiana na wanajeshi.

"Mnaweza mkachezea mikoa yote lakini muilinde Dar es Salaam kama mboni ya jicho. Tukipachafua mtu hawezi kuja Muhimbili, kuleta mazao kwa wafanyabiashara. Watu watashindwa kwenda Ulaya. Tucheze kote lakini hapa kila mmoja apalinde. Mkipachafua mtalala njaa," alisema

**ENEO LA MBEZI**

Katika eneo la Mbezi, wafuasi hao walionekana wakiwa wamevalia sare za chama hicho na bendera, huku wengine wakieleza walifika eneo hilo saa 10:00 alfajiri. Ilipofika majira ya saa 2:00 asubuhi, mamia ya watu walianza kumiminika katika viwanja hivyo eneo lililoandaliwa kwa ajili ya kukutania kuanza maandamano.

Nyimbo na shangwe vilitawala, huku wafuasi wakiwa na mabango yenye ujumbe mbalimbali. Baadhi yalisomeka "Tunataka Katiba Mpya", "Tunataka Bei ya Sukari Ishuke", "Maboresho Sheria za Uchaguzi" na "Serikali Isikilize Hoja za Wananchi".

Ilipotimu saa 4:00 asubuhi, msafara ulianza kwenda ofisi za UN, zilizoko Sinza, Dar es Salaam, huku wafuasi wakiunga safari kwa miguu kutoka Mbezi.

Wakati msafara huo ukifunga barabara nzima na kusababisha foleni, ukihanikizwa kwa nyimbo za chama, pembezoni mwa barabara ya Morogoro ulimokuwa unapita, umati wa watu ulifurika kushuhudia huku baadhi wakiunga mkono kwa kunyoosha vidole viwili, ambayo ni ishara ya CHADEMA.

Maandamano hayo yaliyohusisha kinamama na wazee, baada ya kufika Kibanda cha Mkaa, Lissu aliungana na waandamanaji akitokea uwanja wa ndege. Baada ya kuonekana, shangwe ziliibuka kutoka kwa wafuasi hao.

Lissu na viongozi wengine walitembea kwa miguu hadi Ubungo wakiwa na ulinzi wa polisi, ndipo akapanda gari akawa anaonekana kwa juu huku akisalimiana na wafuasi waliokuwa wamefurika pembezoni mwa barabara.

**BUGURUNI**

Licha ya kuwapo manyunyu, wafuasi walikusanyika majira ya saa 2:30 asubuhi katika eneo la Buguruni, huku Naibu Katibu Mkuu Bara, Benson Kigaila, akitoa mwongozo wa namna gani watakavyoandamana.

Maandamano hayo yalianzia Buguruni yakipita maeneo mbalimbali yakiwamo Ilala, Kariakoo, Fire, Jangwani, Magomeni, Manzese hadi Sinza.

Wakati wafuasi hao wakipokea

Inaendelea Uk.3

VISIT FREE ENTRY
INTL TRADE EXHIBITION ON AGRO & POULTRY - GRAINS
EXHIBITORS FROM AROUND 13 COUNTRIES
AGRO & POULTRY 2024
Intl Trade Show on Aquaculture, Agriculture, Dairy, Irrigation, Livestock & Poultry Tractors, Veterinary Etc.
Products on Display:
Poultry Feed Equipment | Poultry Silo | Feed Tankers | Feed Conveyor Storage | Feed Milling Systems | Metal Cutting | Poultry Slag | Feed Milling Handling | Processing | Silos Poultry Cages & Equipment | Poultry & Dairy Construction Houses | Cage Systems | Egg Grading & Packing | Egg Printing System Feed System & Boilers | Layers Breeding | Animal Feeds & Flour Livestock Feed Supplement Raw Materials | Irrigation Lines | Fittings Equipments | Sprinklers | Vertical Planter | poultry Processing Equipment Slaughterhouse
Grains Africa 2024
International Grains & Technology Trade Exhibition
Products on Display:
Rice Milling Machines | Paddy Seperators | Grain Milling System Feed Milling Systems | Silos | Flour Mill Machinery | Facility-Corn Milling Facility | Semolina Milling | Mills | Feeds & Flour
Date & Venue
26-28 January 2024
Diamond Jubilee Hall, Dar-Es-Salaam - Tanzania
Timing
10:00 AM TO 6:00 PM
For more info, Please Call
0768 616 418 / 0656 482 557

# Cuba, Tanzania wakubaliana ushirikiano katika sekta sita

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI ya Tanzania na Cuba, zimekubaliana kuimarisha ushirikiano katika sekta ya elimu, afya, kilimo, utalii, siasa na michezo.

Makubaliano hayo yalifikiwa jana Ikulu ya Dar es Salaam na viongozi wa serikali hizo kupitia Makamu wa Rais wa Tanzania, Dk. Philip Mpango na Makamu wa Rais wa Cuba, Salvador Valdes Mesa.

Wakizungumza na waandishi wa habari baada ya kutia saini makubaliano ya ushirikiano huo, viongozi hao walisema nchi hizo mbili zimekuwa na historia nzuri ya ushirikiano kwa muda mrefu na watahakikisha wanauendeleza.

Akifafanua kuhusu makubaliano hayo kwenye sekta ya afya, Dk. Mpango, alisema kupitia Wizara za Afya za nchi hizo, wamekubaliana kufanya kila linalowezekana kutumia kiwanda cha viuatilifu cha Kibaha mkoani Pwani kuzalisha dawa zenye ubora kama ilivyo za Cuba.

"Tunafahamu kwamba Cuba imepiga hatua kubwa sana kwa kuzalisha dawa bora zaidi, kwa hiyo tumekubaliana kwamba tushirikiane nao na sisi tuzalishe dawa za namna hiyo," alisema Dk. Mpango.

"Tumefurahi sana kupata fursa ya kujadiliana na kukubaliana kushirikiana katika mambo hayo na serikali hiyo ambayo kwa kweli inafanya vizuri katika maeneo hayo pamoja na teknolojia na haya yote ambayo tumekubaliana na nchi hii yatafanyika kwa Tanzania bara na visiwani."

Alisema Tanzania itaendelea kufanya kila linalowezekana kushinikiza Cuba iondolewe vikwazo vya kiuchumi ambavyo imewekewa kwa muda mrefu.

Makamu wa Rais wa Cuba, Salvador, aliishukuru Tanzania kwa kuendelea kuonesha ushirikiano huo ikiwamo kuendelea kuipambania iondolewe vikwazo hivyo vya kiuchumi ambavyo imewekewa kwa muda mrefu.

Alisema licha ya nchi hiyo kuwekewa vikwazo hivyo, lakini haitakubali kuwa wanyonge bali itaendelea kupambana kujiimarisha kiuchumi kwa kutumia rasilimali zake.

"Na kama mnavyofahamu Cuba imekuwa ikizalisha dawa bora sana na pia ina teknolojia za kisasa, kwa hiyo licha ya vikwazo hivyo tunapambana na tunafanya vizuri kuimarisha uchumi wetu," alisema Salvador.

Viongozi hao walishuhudia utiaji saini wa hati za makubaliano (MoU), kati ya Chuo cha Artemisa Diaza Gonzalez cha Cuba na Chuo cha Kilimo cha Sokoine (SUA) kwa ajili ya ushirikiano kwenye sekta ya kilimo.

Makubaliano mengine ni kati ya Mamlaka ya Dawa Tanzania (TMDA) ya Tanzania na Center for State Control of Medicine Devices (CECMED) ya Cuba kwa ajili ya ushirikiano katika masuala ya dawa na vifaa tiba.

# Historia yawekwa siasa za Tanzania

**Inatoka Uk. 2**

maelekezo ya Kigaila, maofisa wa polisi nao walionekana wakijongea katika eneo hilo kwa lengo la kuimarisha ulinzi, jambo ambalo limepongezwa na wadau mbalimbali.

Kigaila aliwasisitiza wafuasi wa chama hicho kufuata utaratibu uliowekewa ikiwamo kuhakikisha kwamba maandamano hayo yanafanyika kwa amani.

Maandamano yalianza saa 4:00 asubuhi baada ya Mbowe kuwasili huku wafuasi wakiwa na mabango yenye ujumbe "Serikali Iondoe Miswada Mibovu Bungeni", Gharama za Maisha Ziko Juu", Mchakato wa Katiba Uanze Mara Moja" na "Maoni ya Wananchi Yaheshimiwe".

Kama ilivyokuwa kwa barabara ya Morogoro na Sam Nujoma, katika njia walizopita waandamanaji kutoka Buguruni, wananchi walisimama pembezoni na wengine maghorofani.

**OFISI ZA UN**

Katika ofisi za Umoja wa Mataifa (UN) nchini, polisi wenye vyeo vikubwa waliwasili mapema asubuhi huku basi kubwa lenye askari mchanganyiko likipaki kituo cha mafuta kilichoko karibu na eneo hilo.

Kabla ya maandamano kuwasili UN, askari walijipanga katika barabara ya Sinza Makaburini huku wakiweka kituo eneo la Mwika ambako basi la askari na magari mengine yalipaki.

Msafara wa kwanza wa maandamano uliongozwa na Lissu uliwasili UN majira ya saa 9:10 alasiri kupokewa na Muliro pamoja na Mwakilishi wa UN, Zlatan Milisic. Muliro alimpa Lissu utaratibu wa kuingia katika ofisi hizo kwamba wanaohusika ni viongozi wanne wa CHADEMA na raia mmoja.

Lissu alikubaliana na utaratibu huo na kuendelea kumsubiri Mbowe aliyekuwa kwenye msafara uliokuwa unatokea Buguruni ambao uliwasili eneo hilo dakika 11 baadaye.

**WADAU WALONGA**

Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema, alisema polisi wameshirikiana vizuri na raia kiasi cha kuombana maji ya kunywa.

"Sijaona polisi mwenye silaha. wameshirikiana na wananchi kwa namna ya ajabu. Hakuna mtu amepoteza kitu wala aliyejeruhiwa hii maana yake ni kwamba wananchi wanataka mabadiliko bila fujo," alisema.

"Hii ni sifa nzuri kwa Rais Samia Suluhu Hassan, si CHADEMA tu. Watu wana kilio unawaruhusu walie hadharani, inawafanya waishi kwa furaha, ndiyo maana ya maandamano," aliongeza .

Mwanaharakati Dk. Ananilea Nkya, alisema ameungana na wafuasi wa CHADEMA kuwakilisha kundi la watu wasio na vyama kudai katiba mpya, tume huru ya uchaguzi na kushinikiza miswada mitatu ya masuala ya uchaguzi iondolewe bungeni.

Mkurugenzi wa Jukwaa la Katika Tanzania, Bob Chacha Wangwe, alisema waliamua kushiriki maandamano hayo kwa sababu agenda ambazo wanazitumia, wamekuwa wakizipigania, ikiwamo suala la katiba mpya, ugumu wa maisha na kupanda kwa bei za bidhaa.

**Imeandikwa na Restuta James, Halfani Chusi na Maulid Mmbaga.**


UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESEDENT OFFICE,
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
KINONDONI MUNICIPAL COUNCIL

The Kinondoni Municipal Council is pleased to invite expression of interest from investors and public to invest in the development and enhancement of Municipal community parks at **Magomeni** and **Mwananyamala**. We believe that these parks have an immense potential to contribute to the well-being and recreational activities of society residents while creating an attractive environment for visitors. We are seeking partnership from individuals, businessmen and organizations which are interested in investing financially and offering expertise in the development, management, maintenance and operation of the municipal community parks. The aim is to transform these parks into vibrant, safe, and inclusive spaces that cater to the diverse needs of a given community.

These parks have been equipped with all necessary facilities such as electricity, water, toilets/latrines, parking space. The area is covered with green grasses, fencing facility and also interlinked with tarmac roads for all season accessibility.

**Required facilities to be featured in the given parks are:**

1. Park infrastructure development, including kid's playground, sport facilities, walking trails, and seating areas.

2. Landscaping and horticultural enhancement to create visual appealing and environmental sustainable park spaces.

3. Installation of amenities such as fitness equipment, picnic areas, and outdoor gathering spaces.

5. Introduction of innovative programs and activities for community engagement and recreational purposes.

Investors and partners will have the opportunity to contribute to the urban development of Kinondoni

Municipal Council, gaining brand exposure, and making a significant positive impact on the lives of the community members. Interested parties are requested to submit letter of expression of interest highlighting their expertise, proposed investment, and expected outcomes.

**For further inquiries, please contact:**
**KINONDONI MUNICIPAL COUNCIL P.O.BOX 31902**
**MOB: +255 712 222 599 (Contact Person)**

We look forward to receive your expressions of interest and partnering with you to create vibrant, sustainable, and community-centric parks in Kinondoni Municipal Council.

Submission Deadline: **10TH FEBRUARY 2024**

HABARI KITAIFA



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Chama cha Watu Wasioona Tanzania, Castor Kalamera (katikati), akizungumza kwa simu na mtoa huduma wa dawati maalum kwa wateja wenye ulemavu la Vodacom Tanzania Plc, wakati wa uzinduzi wa dawati hilo, katika makao makuu ya kampuni hiyo, Dar es Salaam jana. Wengine ni Mkuu wa Idara ya Huduma kwa Wateja na Kidijitali wa Vodacom, Belinda Wera (kulia) na mfanyakazi mwenye taaluma ya lugha za alama, Godfrey Mhiche. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**


Ujamaa Community Resource Team

EMPOWERMENT JUSTICE STEWARDSHIP

**PO Box 15111, Arusha, Tanzania**
**www.ujamaa-crt.org**

## TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MIRADI

SHIRIKA LA UJAMAA COMMUNITY RESOURCE TEAM NI SHIRIKA LISILO LA KISERIKALI LINALOJISHUGHULISHA NA KUJENGA UWEZO WA JAMII KATIKA MASUALA YA UTAWALA BORA, ARDHI NA MAZINGIRA KATIKA MKOA WA ARUSHA NA MANYARA.

SHIRIKA LINAPENDA KUUTANGAZIA UMMA KUWA LITATEKELEZA MRADI MPYA KAMA INAVYOAINISHWA HAPA CHINI KUANZIA JANUARI 2024 MPAKA DESEMBA MWAKA 2027

UCRT KWA UFADHILI WA INTERNATIONAL UNION FOR CONSERVATION OF NATURE AND NATURAL RESOURCES ITATEKELEZA MRADI UJULIKANAO KAMA ``INCLUSIVE COSERVATION INITIATIVE`` KATIKA WILAYA YAMBULU, LONGIDO, SIMANJIRO, KARATU NA KITETOWENYE THAMANI YA SHILINGI ZA KITANZANIA 3,528,711,209 NA PIA UCRT KWA UFADHILI WA DAUGHTERS FOR EARTH LITATEKELEZA MRADI UJULIKANAO KAMA "STRENGTHENING LAND TENURE SECURITY IN A MAASAI COMMUNITY IN TANZANIA KATIKA WILAYA YA SIMANJIRO KATIKA VIJIJI VYA LOSINYAI NA KANDASIKIRA WENYE THAMANI YA SHILINGI 84,000,000.

MIRADI HII ITATEKELEZWA KWA KUSHIRIKIANA NA HALMASHAURI HUSIKA PAMOJA NA VIJIJI.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI director@ujamaa-crt.or.tzna manager@ujamaa-crt.or.tz.**


# Tatizo uhaba wa sukari kumalizika mwezi Februari

**Na Beatrice Shayo,** aliyekuwa ARUSHA

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, amesema tatizo la sukari linatarajia kumalizika Februari 15 na waliokamatwa kwa kuficha watafikishwa mahakamani wakati wowote.

Kilo moja ya sukari katika baadhi ya maduka nchini ni kati ya Sh. 4,000 hadi 6,000, huku maeneo mengi ikikosekana hali inayowafanya wananchi kukosa huduma hiyo muhimu.

Bashe aliyasema hayo juzi jioni wakati akizungumza na wananchi kwa njia ya simu mkoani Arusha katika ziara ya Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda.

Awali, Makonda alimweleza Waziri Bashe malalamiko ya kupanda sukari na kutaka kujua serikali inafanya jitihada gani nchi inakuwa na sukari ya kutosha.

"Mheshimiwa Bashe habari yako nipo Arusha nimekutana na suala la bei ya sukari tunaomba majibu serikali inafanya nini kuhakikisha tunapata sukari ya kutosha na kwa bei himilivu katika kipindi chote hatutamani kuona sukari inapanda panda," alisema Makonda.

Bashe alisema serikali imechukua hatua baada ya viwanda vya nchini kuathirika katika uzalishaji wameamua kuruhusu uagizaji wa sukari kutoka nje ya nchi.

Alisema shehena ya kwanza itaanza kuingia kuanzia Januari 26 hadi 30, mwaka huu na wametoa vibali vya tani zaidi ya 100,000.

Waziri Bashe alisema Februari 15 hadi 20, mwaka huu hali ya utulivu wa upatikaji wa sukari itakuwapo. "Jambo la pili sio kwamba ndani ya nchi hakuna sukari bali imetokea tabia ya wafanyabiashara ambao tumekuwa tukiwalinda kwa muda mrefu kutengeneza upungufu usiokuwa halali."

Alisema watu wao wameingia kwenye operesheni wamewakamata wanaouaza sukari zaidi ya bei elekezi ambayo haitakiwi kuzidi Sh. 2,700 hadi Sh. 3,200.

"Nimewaomba wakuu wa wilaya na wakuu wa mkoa wakishirikiana na bodi ya sukari kufanya survey (ukaguzi) maeneo yote yanayouza sukari. Kuna wakala wa TPC ambaye alikuwa anauza Sh. 2,700 kwa bei ya jumla hatutarajii kuona sukari Arusha inauzwa Sh. 4,000 hilo jambo halitarajiwi," alionya Bashe.

Kadhalika, alisema juzi imefanyika operesheni kwa Mkoa wa Dar es Salaam, Mwanza na maeneo yote yanayouza sukari kinyume na bei elekezi iliyotolewa na bodi ya sukari, watawachukuliwa hatua na tayari wameshawakamata na wanatarajia kuwafikisha mahakamani.

"Nataka niwahakikishie Watanzania si muda mrefu sukari kutoka nje ya nchi inayotokana na upungufu kwa sababu ya viwanda vimefunga itaingia," alisema Waziri Bashe.

Makonda alisema ipo haja ya kutoa maelekezo kwa maandishi ili kuhakikisha wanaopandisha bei ya sukari ama kufanya ulanguzi akitolea mfano Mkoa wa Mwanza inauzwa Sh. 4,500.

**WANANCHI WANENA**

Lina Masawe, mkazi wa Arusha mjini alisema wanauziwa kwa bei kubwa kati ya Sh. 4,000 hadi Sh. 4,500 kwa kilo hali inayowasababishia maisha kuwa magumu kwa sababu bidhaa nyingi za vyakula zimepanda bei.

Joseph Mollel alisema ni muhimu serikali ikadhibiti hali hiyo ili kuwapunguzia ugumu wa maisha wananchi.

Neema John mkazi wa Mbezi, Dar es Salaam alisema jana alinunua kilo moja kwa Sh. 5,000 ikiwa ni ongezeko la Sh. 2,000 mwezi uliopita.

"Bei ya kilo moja ya sukari inakaribia kilo ya nyama, nimetembea maduka matatu, nimepata kwenye duka moja naye anauza Sh. 5,000 mwezi uliopita nilinunua kwa Sh. 3,500, hali ya maisha inazidi kuwa ngumu, serikali ichukue hatua," alisema.

**MGOGORO WA MASHAMBA**

Waziri wa Mipango na Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo, amesema serikali itahakikisha inatatua mgogoro wa wawekezaji wa mashamba saba ya maua yaliyopo Mkoa wa Arusha ili kuwapa haki zao na kupewa kipaumbele yatakapoanza kazi.

Alisema hayo kwa njia ya simu wakati akijibu swali la Makonda kuwa tathmini imeshafanyika kuhusu mashamba hayo wanafanya mchakato wa kuanza kuyagawa kwa wawekezaji.

**UUZAJI TANZANITE WAIVA**

Kuhusu changamoto ya kizuizi cha kuuza madini ya Tanzanite yaliyotolewa na wananchi, katika mkoa huo na mingineyo, Naibu Waziri wa Madini, Steven Kiruswa, alisema suala la maboresho ya sheria ya madini, limeshafanyika na utaratibu unaendelea kulikamilisha kuruhusu kuuzwa.

Alisema Ofisi ya Waziri na Mwanasheria Mkuu wanaendelea kufanyia kazi mabadiliko hayo ya sheria ifikapo Januari 28, litakuwa limekamilika na wananchi kuruhusiwa kuuza madini hayo.

**MITA ZA MAJI**

Wanananchi walilalamikia kero ya kubambikiziwa bili za maji, kupewa maji yenye chumvi na wakati mwingine kukosekana huduma hiyo.

Makonda alimpigia simu Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, ambaye aliagiza wasoma mita kutosoma bili za maji bila kushirikisha wananchi na kuahidi kufika Arusha kutembelea vyanzo vya maji kubaini uwapo wa chumvi katika maji hayo.



# Aongezwa kesi ya uchakachuaji EFD

**Na Grace Gurisha**

UPANDE wa mashtaka katika kesi ya uhujumu uchumi namba 8 ya mwaka 2023 yenye mashtaka saba, ikiwamo kuisababishia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) hasara ya Sh. milioni 954.5, inayowakabili mafundi wa mashine za kielektroniki (EFD) umefanya mabadiliko hati ya mashitaka kwa kumwongeza mfanyabiashara Frank Kalage.

Washtakiwa wengine ni Awadhi Mhavile, Ally Msesya maarufu kama Ally Yanga (37) mafundi wa mashine za EFD na Salma Ndauka (38) msimamizi wa gereji.

Mshtakiwa Kalage alisomewa mashtaka manne jana kati ya saba mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Mfawidhi Is-hqa Kuppa wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Job Mrema, akisaidiana na mawakili wa serikali Emmanuel Medalakini na Auni Chilamula.

Kalage ameunganishwa kwenye mashtaka ya kutumia isivyo halali mashine za EFD zilizozuiwa na kumpotosha Kamishna wa kodi, kumdanganya Kamishna Mkuu wa TRA kwa kutoa risiti zisizo sahihi na kuwanufaisha walipakodi wengine kudai Sh 954,596,372, hivyo kuisababishia TRA hasara na utakatishaji fedha.

Mrema alidai kuwa washtakiwa walitenda makosa hayo kati ya Mei na Julai, 2023 ndani ya jiji la Dar es Salaam.

Ilidaiwa kuwa kati ya Mei 17 na Julai 2023, katika maeneo tofauti jijini Dar es Salaam, washtakiwa wote kwa pamoja walitumia isivyohalali mashine za EFD zilizozuiwa kinyume na sheria kutengeneza risiti zisizo halali zilizopakiwa kwenye mfumo wa TRA na kuwezesha walipa kodi wengine kudai Kodi ya Ongezeko la Thamani ya Sh 954,596,372 na kumpotosha Kamishina Mkuu wa mamlaka hiyo.

Pia washtakiwa wote kwa pamoja wanadaiwa kutumia isivyo halali mashine za EFD zilizokuwa zimefungiwa na kumdanganya Kamishna wa TRA kwa kutoa risiti zisizo sahihi, hivyo kuwanufaisha walipakodi wengine kudai Sh 954,596,372.

Aidha katika shtaka la tatu linalomkabili Mhavile peke yake, inadaiwa kuwa Julai 8, 2023, mshatakiwa alikutwa na mashine za 22 za EFD zinazodhaniwa kuwa za wizi au zilizopatikana kwa kwa njia isiyo halali.

Wakili alidai kudai kuwa, Julai 19, mwaka jana maeneo ya Sinza A, Ubungo mkoani Dar es Salaam, Ndauka alikutwa na mashine 10 za EFD zidhaniwazo kuwa za wizi au kuchukuliwa kwa njia ya isiyo halali.

Mshtakiwa Mhavile anadaiwa pia Julai 8, 2023 maeneo ya Lumumba mkoani Dar es Salaam, alikutwa na mashine 10 za EFD na kutoa risiti za kielektroniki kinyume na sheria.

Aliendelea kudai kuwa washtakiwa wote kwa pamoja kati ya Mei 13 na Julai, 2023 mkoani Dar es Salaam, waliisababishia serikali (TRA) hasara ya Sh. milioni 954.5.

Katika mashitaka ya utakatishaji fedha, inadaiwa kati ya Mei 13 na Julai, 2023 jijini Dar es Salaam, washtakiwa wote kwa kutumia mashine hizo walitoa risiti zisizo halali zilizotumiwa na walipakodi wengine kudai Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ya Sh. milioni 954.5 TRA wakati wakijua kwamba fedha hizo ni zao la kosa la kuisababishia serikali hasara.

Mshtakiwa huyo hakuruhusiwa kujibu chochote mahakamani hapo kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi hadi kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashitaka (DPP).

Kwa mujibu wa upande wa mashtaka, upelelezi wa shauri hilo bado haujakamilika na hakimu Kuppa ameahirisha kesi hiyo hadi Februari 7, mwaka huu, na washtakiwa wataendelea kukaa rumande kwa kuwa mashtaka hayo hayana dhamana kisheria.

# Rais Samia ziarani Indonesia

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS Samia Suluhu Hassan, yuko nchini Indonesia kwa ziara ya siku tatu.

Kupitia akaunti yake ya Instagram, Rais Samia aliandika kwamba yuko Indonesia kwa mwaliko wa Rais wa nchi hiyo, Joko Widodo.

"Nimewasili nchini Indonesia kwa ziara ya kitaifa ya siku tatu, kufuatia (kutokana na) mwaliko wa kaka yangu Mheshimiwa Rais Joko Widodo,"aliandika Rais Samia.

Alisema uhusiano wa nchi hizo mbili Januari 13, mwaka huu ulitimiza miaka 59 tangu ulipoanzishwa, ukiwa na tija kwa Tanzania.

"Uhusiano wa Indonesia na Tanzania umekuwa na tija kwa mamilioni ya Watanzania hasa kwenye kilimo na biashara. Tunaendelea kufanya kazi ya kukuza uhusiano huu ili kuleta tija zaidi kiuchumi kwa nchi yetu," alisema Rais Samia.

Baadhi ya wananchi wanaomfuatilia kwenye mtandao huo, walitoa maoni yao kuhusiana na ziara hiyo.

Halima alisema: "Hongera mama kila la kheri. Kilimo ni biashara, ugundue mengi katika kuendeleza kilimo hasa soko la mazao. Wenzetu wanaendeshaje ili wananchi wako tunufaike na kilimo. Kilimo ni utajiri."

"Kila la heri mheshimiwa Rais katika majukumu yako. Iwe na mafanikio kwa mataifa yetu mawili,"aliandika hivyo Consultance Alive.

Rajabu Singano aliandika: "Sawa mama tuko nyuma yako tutafutie ugali na huku tunaendelea na usafi, nchi iko salama."

"Kila la kheri mheshimiwa, tuko nyuma yako endelea kulipambania taifa mkuu," aliandika Mohammed.

Miongoni mwa mambo yanayotiwa mkazo na serikali ya awamu ya sita ni kukuza diplomasia ya uchumi na Rais Samia amekuwa akisafiri nje ya nchi kuhamasisha na kutekeleza jambo hilo kwa vitendo.

Rais Samia amekuwa akishuhudiwa akikutana na mamlaka na jumuiya za wawekezaji na wafanyabiashara katika nchi anakotembelea kuvutia uwekezaji kutoka nchi nyingine kuja kuwekeza nchini.

Kwa mujibu wa Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Rais Samia anafanya ziara ya siku tatu katika nchi hiyo ya Indonesia.


halotel

TAARIFA KWA UMMA

Viettel Tanzania PLC (Halotel) ni kampuni ya mawasiliano inayoendelea kuboresha huduma na kuvunja mipaka ya mawasiliano kwa wateja wetu kwa kutoa gharama nafuu kwenye SMS, Huduma za kupiga simu na Intaneti.

Tunapenda kuwatangazia wateja wetu na umma kwa ujumla juu ya gharama zetu za makato pindi mteja atakapokuwa hajajiunga kwenye kifurushi.

GHARAMA ZA NDANI YA NCHI

| Kipengele | Gharama |
|---|---|
| Kupiga Halotel kwenda Halotel | 10 Tsh/Dk |
| Kupiga Halotel kwenda mitandao mingine | 20 Tsh/Dk |
| Kutuma SMS | 5 Tsh/SMS |
| Data (MB) | 9.35 Tsh/MB |

GHARAMA ZA NJE YA NCHI

GHARAMA ZA KUPIGA SIMU NJE YA NCHI

| Kanda | Gharama (Tsh/Dk) |
|---|---|
| **Ukanda 1:** USA, UK, India, China, Canada, Australia, Japan, South Korea, Vietnam, Laos, Cambodia | 450 |
| **Ukanda 2:** Nchi nyingine za ULAYA, Kenya | 750 |
| **Ukanda 3:** Rwanda, Afrika Kusini, Zambia, UAE, Oman,Haiti, Peru | 840 |
| **Ukanda 4:** Cameroon, Zimbabwe, Malawi, Uganda, Congo DRC, Mozambique | 1,000 |
| **Ukanda 5:** Burundi | 1,350 |
| **Ukanda 6:** Sehemu nyingine duniani | 2,700 |
| **Ukanda 7:** Mitandao ya satelite | 13,800 |

GHARAMA ZA KUTUMA SMS NJE YA NCHI

| SMS | Gharama |
|---|---|
| SMS kwenda nje ya nchi | 95 Tsh/SMS |

| Aina ya kifurushi | Muda | Gharama (Tsh) | Mitadao Yote (Dk) | Halotel-Halotel (Dk) | SMS | Data (MB) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| VIFURUSHI VYA SAUTI | | | | | | |
| Dakika & SMS | Siku | 350 | 25 | | | |
| Dakika & SMS | Siku | 500 | | 110 | | |
| Dakika & SMS | Siku | 500 | 60 | | 60 | |
| Dakika & SMS | Siku | 1,000 | 180 | | 60 | |
| Dakika & SMS | Siku 2 | 1,000 | 160 | | 25 | |
| Dakika & SMS | Siku | 700 | 10 | Kila Dk 5 za mwanzo bure | | |
| Dakika & SMS | Wiki | 1,500 | 180 | | 150 | |
| Dakika & SMS | Wiki | 2,500 | 350 | 50 | 150 | |
| Dakika & SMS | Wiki | 3,000 | 450 | | 150 | |
| Dakika & SMS | Mwezi | 4,000 | 400 | 50 | 50 | |
| Dakika & SMS | Mwezi | 5,000 | 550 | 650 | 100 | |
| Dakika & SMS | Mwezi | 10,000 | 1,600 | 1,600 | 150 | |
| Dakika & SMS | Bila Kikomo | 500 | 20 | | | |
| VIFURUSHI VYA SMS | | | | | | |
| SMS | Siku | 100 | | | 200 | |
| SMS | Wiki | 500 | | | 2000 | |
| SMS | Mwezi | 1,000 | | | 10,000 | |
| VIFURUSHI VYA INTANETI | | | | | | |
| Intaneti | Siku | 350 | | | | 170 |
| Intaneti | Siku | 500 | | | | 245 |
| Intaneti | Siku | 1,000 | | | | 490 |
| Intaneti | Siku | 2,000 | | | | 985 |
| Intaneti | Siku 10 | 2,100 | | | | 1024 |
| Intaneti | Wiki | 1,000 | | | | 490 |
| Intaneti | Wiki | 2,000 | | | | 985 |
| Intaneti | Wiki | 3,000 | | | | 1475 |
| Intaneti | Wiki | 5,000 | | | | 2460 |
| Intaneti | Wiki | 10,000 | | | | 4925 |
| Intaneti | Mwezi | 10,000 | | | | 4920 |
| Intaneti | Mwezi | 20,000 | | | | 9850 |
| Intaneti | Mwezi | 30,000 | | | | 14780 |
| Intaneti | Mwezi | 50,000 | | | | 24600 |
| VIFURUSHI VYA COMBO | | | | | | |
| Combo | Wiki | 2,000 | 55 | | 20 | 850 |
| Combo | Wiki | 2,500 | 20 | | 20 | 1150 |
| Combo | Wiki | 3,000 | 100 | | 30 | 1250 |
| Combo | Siku 10 | 3,100 | 150 | 20 | 300 | 1024 |
| Combo | Mwezi | 10,000 | 280 | | 50 | 4000 |
| Combo | Mwezi | 20,000 | 400 | | 100 | 8500 |
| Combo | Mwezi | 50,000 | 600 | | 200 | 22000 |

Halotel Tanzania Halotel_Tanzania

www.halotel.co.tz

*Vigezo na masharti kuzingatiwa

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Historia imeandikwa, kumbe inawezekana

**KITENDO** cha Jeshi la Polisi kuruhusu maandamano ya amani ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na kuahidi kuyalinda, kimeleta sura mpya ya demokrasia nchini na kinapaswa kuwa mfano wa kuigwa hata na nchi nyingine za Afrika.

Maandamano kama haya ya vyama vya upinzani, mara nyingi yalikuwa hayapewi nafasi kwa kuhofia kutokea vurugu.

Pongezi kubwa zimwendee Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye ndiye Amiri Jeshi Mkuu kwa kuruhusu demokrasia itawale nchini.

Kuruhusiwa kufanyika kwa maandamano hayo ya amani bila shaka hakukutarajiwa kutoka kwa viongozi wa chama na wanachama wa chama hicho kutokana na historia iliyozoeleka miaka ya nyuma ya kuzuiliwa kila wanapoomba kufanyika.

Kumbe kila jambo linawezekana ilimradi tu sheria na taratibu zinapofuatwa kwa pande zote mbili, kutoka kwenye vyama vyenyewe na upande wa vyombo vya dola ambavyo vinalinda usalama wa nchi.

Maandamano ya jana yanatoa funzo kuwa kila jambo linawezekana kama kutakuwapo na mwafaka wa kinachokwenda kufanyika.

Kupitia maandamano wananchi hupata fursa ya kutoa dukuduku zao na serikali jukumu lake ni kuchukua na kufanyia kazi.

Maandamano ya jana yamedhihirisha kuwa wananchi na wafuasi wa vyama vya upinzani wanaweza kuwasilisha hoja zao kwa njia ya amani bila kutumia nguvu na vurugu zisizo na sababu ambazo matokeo yake husababisha vifo, majeruhi na kuharibu taswira ya nchi.

Mara nyingi yanapotokea maandamano, kuna watu ambao hutumia fursa hiyo kufanya maovu ili walioandaa waonekane wao ndio walioanzisha.

Pongezi pia kwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, kwa kuungana na wanachama wa CHADEMA na wananchi wengine katika maandamano hayo ya amani.

Wakati wa maandalizi ya kufanyika kwa maandamano hayo kulianza kuzuka sintofahamu ya kutoruhusiwa kufanyika. Hata hivyo, Jeshi la Polisi chini ya Kamanda wake Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Murilo, liliruhusu maandamano hayo na kuahidi kuyalinda katika barabara zote zilizotangazwa kuwa yatapita.

Katika barua ya Jeshi la Polisi ya kuruhusu maandamano hayo, iliwataka viongozi wa CHADEMA kubeba jukumu la kuzuia lugha za uchochezi, kejeli ambazo zinaweza kusababisha kutendeka kwa vitendo vya uvunjifu wa sheria.

Chama hicho kilitakiwa kufuata utaratibu wa kisheria katika maeneo yote kwa kadri watakavyoelekezwa na wasimamizi wa sheria, polisi wakiwa ni kiongozi katika eneo wanalolitolea taarifa.


Aidha, Jeshi la Polisi lilionya maandamano hayo yasisababishe uvunjifu wa amani, watu kuibiwa au kuporwa na yafanyike kwenye njia zilizokubaliwa na muda waliopanga bila kuingizwa mambo mengine yaliyo nje ya makubaliano yaliyofanyika katika kikao chao na chama hicho.

Jeshi hilo lilionya pia ukiukwaji wowote wa masharti hayo utalilazimisha jeshi la polisi kuchukua hatua za kisheria bila kusita ili kuzuia madhara ya kuvunjika kwa amani.

CHADEMA wakati wakiandaa maandamano hayo walisema wanataka kuishinikiza serikali kuondoa bungeni miswada mitatu inayohusu vyama vya siasa na uchaguzi, kikidai kuwa baadhi ya vipengele vinakosolewa na chama hicho ambayo tayari imeshawasilishwa bungeni ukiwamo wa tume huru ya uchaguzi.

Maandamano bila vurugu yanawezekana, hili liwe funzo kwa wengine na kuiga kutoka Tanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Mary Seme

# Kongole Bakita kukipaisha Kiswahili kimataifa, tuko pamoja kwa yote

**NI** dhahiri kadri siku zinavyokwenda mbele, lugha ya Kiswahili nayo inazidi kusonga na kutambulika kimataifa.

Nilipongeze Baraza la Kiswahili Taifa (BAKITA) kwa kutoa wito kwa vijana waliobobea katika lugha adhimu ya Kiswahili, kutumia fursa hii katika nchi za EAC zikijumisha Kenya, Uganda, Burundi, Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia Congo (DRC), Somalia, Sudan Kusini pamoja na Tanzania.

Rai hii ilitolewa na BAKITA baada ya kuona kuwapo hitaji la wakalimani katika nchi za Afrika Mashariki, hivyo inawataka Watanzania wenye taaluma kuweza kuchangamkia fursa hiyo, kwani si kila anayejua lugha ya Kiswahili anaweza kushiriki, bali ni wale wenye taaluma hiyo, ndio wanaweza kushiriki katika fursa hii.

Mnamo Januari 9 mwaka huu, Katibu Mkuu wa EAC, Dk. Peter Mathuki, alipohojiwa na Idhaa ya Kiswahili Umoja wa Mataifa, alisema utekelezaji unaanza rasmi kutumika kwa Kiswahili kama mojawapo ya lugha rasmi katika jumuiya hiyo.

"Imepitishwa na ina fungu la kuwezesha lugha tatu kutumika ambazo ni Kingereza, Kifaransa na Kiswahili, bajeti yetu ya mwaka huu, tumeweka mikakati yote kuwa na watafsiri wa makabrasha yote.

"Tuwaajiri wataalamu wa Kiswahili, pia kwa lugha ya Kiingereza, Kiswahili na Kifaransa," alisema Dk. Mathuki.

Katika kuliona hilo, baraza pia limewataka waliobobea katika lugha ya Kiswahili, waanza kujiandaa katika kushiriki mafunzo ya ukalimani pamoja na kufundisha lugha ya Kiswahili kwa wageni.

Ili kufanikisha suala hilo, ni vyema serikali kwa kushirikiana na wadau wa lugha adhimu ya Kiswahili, kuanza kuwapa kipaumbele wanafunzi pamoja na wadau wengine wa Kiswahili, huku wakizingatia taaluma yao ya Kiswahili.

Ni dhahiri kwamba wapo wanafunzi wengi waliohitimu shahada na stashahada za Kiswahili na hawana ajira, ni fursa basi kwao kuweza kushiriki katika nchi za EAC, maana idadi yake ni nane, si haba, hasa walipotangaza kuanzia nchini Sudan inayohitaji wakalimani wa Kiswahili.

Ni fursa kwenu vijana kuanza kuchangamkia fursa hii kueneza Kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki, pia kujipatia ajira kupitia lugha hiyo.

Niwadokeze si jambo jipya, mwanzoni mwa miaka ya 1990, Kenya iliomba wataalamu wa ngazi ya vyuo vikuu na wakawapata wengi tu nchini.

Katibu Mtendaji BAKITA, Consolata Mushi alipozungumza na Nipashe wiki iliyopita, alisema kwa kauli hiyo ni kwamba utekelezaji unaanza rasmi, licha ya awali kufahamika lugha hiyo imekwishatolewa taarifa ya kutumika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

"Ni fursa kwa wakalimani wetu kwenye soko hili la EAC, pamoja na kwamba tayari ulikwishafanya kazi ya ukalimani na EAC, ila haikuwa rasmi sana kwa tamko hilo ni kwamba utekelezaji utaanza rasmi 2024," alisema Consolata.

Kiswahili kilitangazwa rasmi kutambuliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu Sayansi na Utamaduni (UNESCO) na kila mwaka Julai 7, dunia inaadhimisha siku hiyo.

"Kiswahili tunakitegemea sana sababu wananchi wengi katika jumuiya yetu wanaelewa lugha ya Kiswahili kwa hiyo, hii sasa itakuwa kazi yetu sisi kama watendaji wa jumuiya kuhakikisha kwamba habari zote na vikao vyote vinafanyika kwa lugha ya Kiswahili," alisema Mushi.

Najua mengi yamefanyika huko nyuma, kuanzia na Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere, akaifanya lugha ya kujifunza darasani kwa elimu ya msingi.

Wanazuoni kama waliopo katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, nao wakamuuga mkono siku nyingi Mwalimu Nyerere kwa kuundwa Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) na sasa imebadilishwa kuitwa TATAKI kwa maana ya Taasisi ya Taaluma ya Kiswahili, ambayo ni mdau makubwa wa BAKITA.

Niseme, hilo katika maisha ya kila siku, kutoa redioni kuwapo vipindi maalum vya Kiswahili vinavyodumu hadi leo, hata kufanya ninachohimiza ni kuendeleza kilichoanza siku nyingi, ikiwa ni sehemu ya uwekezaji kijamii, baada ya uhuru wa nchi. Kongole kwa yote yanayoendelezwa kwenye lugha hiyo adhimu kimataifa.

# Sekta ya maji yaongoza kulalamikiwa 2024

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

MALALAMIKO yanayohusu sekta ya maji yameongoza kuripotiwa kwenye baraza la ushauri la watumiaji wa huduma za nishati na maji, EWURA CCC, katika kipindi cha kufikia Januari 2024 kati ya 15,131 yaliyowasilishwa, 7,515, yalihusu maji, 396 umeme na mafuta na gesi ya kupikia majumbani yakiwa ni malalamiko 161.

Hayo yalibainishwa na Kaimu Katibu Mtendaji wa EWURA CCC, Stelah Lupimo, wakati wa mkutano wa kuwajengea uwezo wajumbe wa kamati za watumiaji za mikoa, na kubainisha wameendelea kuwasaidia watumiaji kuwasilisha ama kulalamika kwa niaba yao changamoto zinazohusu sekta hiyo.

Alisema katika kipindi hicho, Baraza hilo ambalo limeanzishwa kwa mujibu wa sheria chini ya kifungu namba 30 cha Sheria ya EWURA, sura ya 414, limelenga pamoja na mambo mengine kulinda maslahi ya watumiaji wa huduma za nishati na maji, limeendelea kuwajengea uelewa watumiaji kuhusu haki na wajibu wao.

"Tumekuwa pia tukihamasisha umma kushiriki na kuchukua hatua mbalimbali katika masuala ya udhibiti, ikiwamo ushiriki wa wadau kwenye mikutano ya taftishi inayoandaliwa na kuitishwa na mdhibiti, kufanya tafiti zinazolenga kufahamu hali ya upatikanaji wa huduma kwenye maeneo yao na pengine kuishauri serikali, mdhibiti na watoa huduma," alisema Lupimo.

Kadhalika, katika utendaji wao wa kazi wamekutana na mafanikio na changamoto ikiwamo kuanzisha kamati 30 kwenye mikoa 26 ya Tanzania Bara, kuongeza ofisi kutoka nane mwaka 2014 hadi 21 katika mikoa yote ya bara, kufanya progamu 7,324 za uelimishaji na kuwafikia watu 895,126 kutoka misaada ya kisheria kwa walalamikaji wakati wa kusikiliza mashauri yao na mikutano ya mwaka ya kamati.

Hata hivyo, alisema bado wanakabiliwa na changamoto ya kifedha kutokana na utegemezi wa chanzo kimoja cha mapato, kushindwa kufungua ofisi kila mikoa na kushindwa kuajiri pamoja na uhaba wa vitendea kazi ingawa wameanza kazi ya kubaini vyanzo tofauti vya fedha kwaajili ya utekelezaji wa majukumu yake.



Akimwakilisha Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Dk. James Andalile, Meneja wa mamlaka hiyo Kanda ya Mashariki, Musira Nyirabu, aliwapongeza wajumbe wa kamati hiyo kwa kazi kubwa wanayofanya kwa kujitolea, kutetea Watanzania katika maeneo wanakoishi ili watoa huduma za nishati na maji watoe kwa ubora unaokubalika.

Pia, aliwahimiza watoa huduma za nishati na maji ikiwamo mamlaka za maji na TANESCO nchini pamoja na vituo vya mafuta kutoa ushirikiano wa dhati kwa baraza la EWURA CCC, na wajumbe wa kamati za mikoa ili kwa kushirikiana waweze kutatua changamoto za wananchi.

Aliiahidi mamlaka hiyo kama mdhibiti itaendelea kutoa ushirikiano wa hali na mali ili majukumu ya kamati hizo na baraza yaweze kufikiwa kwa ufanisi na kuwasihi kuendelea kujizatiti kutoa elimu kwa wananchi ili kuongeza uelewa kuhusu haki na wajibu wao na kufanya maamuzi na matumizi sahihi na endelevu ya huduma za nishati na maji na kuchangia kuboresha huduma hizo.

"Bado Kamati nyingi hazijaanza kufikisha huduma maeneo ya wilayani, ni maelekezo yangu kwa baraza liendelee kutafuta vyanzo zaidi ya fedha ili kuziwezesha kamati hizi kupanua wigo wake wa utoaji elimu hadi ngazi za wilaya," alisisitiza.

Alisema ni jambo lisilopaswa kubezwa kuwa bado kuna watumiaji wengi hawana uelewa wa kutosha kuhusu haki na wajibu wao, na hata wanapokuwa hawaridhishwi na huduma wengi wao huwa hawaelewi ni wapi pa kulalamika ama mfumo gani watumie kuwasilisha malalamiko yao.

"Tumeshuhudia watumiaji wengi wa huduma za nishati na maji wakipeleka malalamiko yanayohusu huduma hizo kwa wenyeviti na watendaji wa kata na pengine wakuu wa wilaya, wabunge au polisi, hii inaonesha kuwa bado elimu kuhusu uwasilishaji wa malalamiko na utatuzi wake kwa upande wetu haijafikishwa kwa watumiaji ipasavyo, mjikite kufikisha elimu hii kwa wananchi," alisema.

Mwenyekiti wa EWURA CC Mhandisi David Ngula, aliwasihi wajumbe wa kamati za mikoa kutumia nafasi zao kuelimisha jamii kutambua haki na wajibu wao na namna sahihi ya kuwasilisha malalamiko ili kushiriki kutekeleza moja ya majukumu ya baraza hilo ya kutoa elimu kwa wadau.


## TANGAZO/ NOTISI YA MNADA WA HADHARA

**LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD,** kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na **MWANGA HAKIKA BANK LIMITED**, tutauza kwa njia ya Mnada wa hadhara mali/dhamana za mdaiwa wake kama ilivyo onyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utafanyika mahali dhamana zilipo baada ya Siku saba (7) kama rudio la tangazo kuanzia tarehe ya Notisi /Tangazo hili endapo hawatalipa madeni yao.

| NA | JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE NA SAA YA MNADA | KAMPUNI/DALALI HUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | SALUM OMARI AMIRI | LATIFA M. MLANZI | HATI YA MAUZIANO ILIYOTOLEWA NA SERIKALI YA MTAA | UPEMBENI MWANDEGE, MKURANGA,MANISPAA YA ILALA | TAREHE NI KUANZIA 02/02/2024 NA KUENDELEA<br>MUDA NI KUANZIA SAA 04;00 ASUBUHI NA KUENDELEA | LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi wa dhamana unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mali/dhamana itauzwa katika hali iliyopo na mahali ilipo.
3. Mshindii wa mnada atalazimika kulipa malipo yasiyopungua 25% ya bei iliyofikiwa siku yamnada, na 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa na bank (eviction) ni za mnunuzi.
5. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti moja wapo hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

**TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED**
**P.O.BOX 1305**
**Songea, Ruvuma**
**Tel: 0757 940 064/ 0716 070 298 / 0784 718 734**
**Email: twinscoltd5@gmail.com**

# Nchimbi ataja sifa za kiongozi anayefaa kwenye chama

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Emmanuel Nchimbi, amesema viongozi wa chama hicho wanatakiwa kufanana na chama chao kimaadili na kiutendaji na kuheshimu watu.

Alisema viongozi wanaotaka kuchaguliwa na Chama hicho wanatakiwa kujitengeneza kufanana na wanaokubalika kwa watu.

Alisema hayo jana mjini Kibaha alipokuwa anazungumza na wanachama wa CCM waliofika kumpokea katika Shule ya Uongozi ya Mwalimu Nyerere na kuungana na makatibu wengine kutoka vyama vya ukombozi Kusini mwa Afrika.

"Isifike mahala unakutana na wanachama wanavyokutambulisha kama huyu ni kiongozi wa chama wanaanza kusema huyu nikikutana naye siku za hivi karibuni badala ya kutaja cheo chake," alisema Nchimbi.

Alisema wanachama wanatakiwa kuchagua viongozi wenye sifa wanaoweza kukitetea chama wenye kuleta heshima ndani ya chama hicho.

Aliwataka kutoona haya kukitetea chama chao mambo ambayo kimefanya kwa kuwa hakuna chama kinaweza kufanya hivyo.

"Zipo nchi nyingine watu wanahagaika wanakusanya kodi wengine wanachota wanafanya mambo yao na umaskini unatawala tofauti na CCM yetu," alisema.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Pwani, Mwinshehe Mlao, alisema walipata taarifa ya ujio wake wakaamua kumfanyia mapokezi kwani ni mara yake ya kwanza kufika katika mkoa huo akiwa kama Katibu Mkuu.



Mwanasheria wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Wakili Kessy Mponela (kulia), akitoa mafunzo ya kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati ya Watumiaji Mikoa, kuhusu majukumu ya mamlaka hiyo, kwenye nishati na maji, yaliyoratibiwa na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC), mjini Morogoro jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mshitakiwa aongezwa kesi ya uhujumu uchumi

**Na Grace Gurisha**

UPANDE wa mashitaka katika kesi ya uhujumu uchumi yenye mashtaka saba likiwamo la kuisababishia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) hasara ya Sh. milioni 954.5 inayowakabili mafundi wa mashine za kielektroniki za EFD, umefanya mabadiliko kwa kumwongeza mfanyabiashara Frank Kalage.

Washtakiwa wengine ni Awadhi Mhavile, Ally Msesya maarufu kama Ally Yanga (37) mafundi wa mashine za EFD na Salma Ndauka (38), msimamizi wa gereji.

Mshitakiwa Kalage alisomewa mashitaka manne jana kati ya saba mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Is-hqa Kuppa wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam na Wakili wa Serikali Mwandamizi Job Mrema, akisaidiana na Wakili wa Serikali Emmanuel Medalakini pamoja na Auni Chilamula.

Kalage ameunganishwa kwenye mashitaka ya kutumia isivyohalali mashine za EFD zilizozuiwa na kumpotosha Kamishna wa kodi, kumdanganya Kamishna wa TRA kwa kutoa risiti zisizo sahihi na kuwanufaisha walipa kodi wengine, kudai Sh. 954,596,372, kuisababisha TRA hasara na utakatishaji fedha.

Mrema alidai kuwa washitakiwa wametenda makosa hayo kati ya Mei na Julai mwaka 2023, jijini Dar es Salaam.

Ilidaiwa kuwa kati ya Mei 17 na Julai 2023, katika maeneo tofauti ya jiji hilo, washitakiwa wote kwa pamoja walitumia isivyohalali mashine za EFD zilizozuiwa kinyume na sheria kutengeneza risiti zisizo halali zilizopakiwa kwenye mfumo wa TRA na kuwezesha walipa kodi wengine kudai Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ya Sh. 954,596,372 na kumpotosha Kamishina wa mamlaka hiyo. Pia, washitakiwa wote kwa pamoja wanadaiwa kutumia isivyo halali mashine za EFD zilizokuwa zimefungiwa na kumdanganya Kamishna wa TRA kwa kutoa risiti zisizosahihi na kuwanufaisha walipa kodi wengine kudai Sh. 954,596,372.

Katika mashitaka matatu yanayomkabili Mhavile, inadaiwa, Julai 8, 2023, mshitakiwa huyo alikutwa na mashine za kielektroniki 22 zinazodhaniwa kuwa za wizi au zimepatikana kwa njia isiyo halali.

Wakili alidai kuwa Julai 19, mwaka jana, maeneo ya Sinza A, Wilaya ya Kinondoni, Ndauka alikutwa na mashine 10 za EFD zidhaniwazo kuwa za wizi au kuchukuliwa kwa njia ya isivyohalali. Mshtakiwa Mhavile anadaiwa pia Julai 8, 2023 maeneo ya Lumumba mkoani Dar es Salaam, alikutwa na mashine 10 za EFD na kutoa risiti za kielektroniki kinyume na sheria.

Aliendelea kudai kuwa washitakiwa wote kwa pamoja kati ya Mei 13 na Julai mwaka 2023, mkoani Dar es Salaam, washitakiwa Mhavile, Ndauka na Msesya waliisababishia serikali (TRA) hasara ya Sh. milioni 954.5.

Katika mashitaka ya utakatishaji fedha, inadaiwa kati ya Mei 13 na Julai mwaka 2023, jijini Dar es Salaam, washitakiwa wote kwa kutumia mashine hiyo walitoa risiti zisizohalali zilizotumiwa na walipakodi wengine kudai VAT ya Sh. milioni 954.5 kwa TRA wakati wakijua kwamba fedha hizo ni zao la kosa la kuisababishia serikali hasara.

Hata hivyo, mshitakiwa huyo hakuruhusiwa kujibu kitu chochote mahakamani kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi hadi kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashitaka nchini (DPP).

Kwa mujibu wa upande wa mashtaka upelelezi wa shauri hilo bado haujakamilika na hakimu Kuppa aliahirisha kesi hiyo hadi Februari 7, 2024. Washitakiwa wataendelea kukaa rumande kutokana na mashitaka hayo kutokuwa na dhamana.

## TIC yawahamasisha Watanzania miradi ya ubia

**Na Joseph Mwendapole**

KITUO cha Uwekezaji Nchini (TIC), kimewahamasisha Watanzania kuunganisha nguvu ya mitaji na kusajili miradi ya ubia kwenye kituo hicho kama inavyofanya kwa baadhi ya wawekezaji wa kigeni.

Wito huo ulitolewa jana mkoani Morogoro na Mkurugenzi wa Mipango Utafiti na Mifumo ya kompyuta wa TIC, Revocatus Rasheli.

Alikuwa akizungumza na wafanyabiashara katika mwendelezo wa kampeni ya kitaifa kuhamasisha uwekezaji wa ndani iliyozinduliwa rasmi hivi karibuni na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Kampeni hiyo inayotarajiwa kukamilika Septemba, mwaka huu, inalenga kuhamasisha Watanzania kutumia fursa za uwekezaji zilizopo nchini na waache fikra kuwa uwekezaji ni kwaajili ya wageni pekee.

Revocatus alisema Tanzania imebarikiwa kuwa na fursa nyingi ambazo Watanzania wanapaswa kuchangamkia na iwapo wataunganisha mitaji yao wanaweza kufanya mambo makubwa.

"Sisi bado tunaendelea na kampeni kwenye mikoa mbalimbali nchini na mpaka sasa tumeshapitia mikoa 12 tunakutana na wananchi tunawaeleza fursa zilizopo na namna ambavyo serikali inatoa kipaumbele kwa wawekezaji Watanzania," alisema.

Aliwaeleza wafanyabiashara wa mkoani Morogoro kwamba serikali imepunguza kiwango cha mtaji kwa mwekezaji mtanzania kutoka Dola za Marekani 100,000 hadi dola 50,000 ili kuwezesha Watanzania wengi kuwekeza.

"Na Watanzania wafahamu kwamba tunaposema dola 50,000 haimaanishi kwamba ni fedha taslimu, huu ni mtaji kwa ujumla wake kuanzia mashine mitambo kama ni eneo la uwekezaji vyenye thamani kama hiyo na siyo fedha taslimu," alisema.

Juzi maofisa wa TIC walitembelea miradi mkoani Morogoro inayohusu utengenezaji wa chakula cha wanyama, International Tanfeed Limited na Kiwanda cha Sukari, Kilosa – Dakawa.

Akizungumza kwenye kiwanda cha Tanfeed ambacho ni cha mtanzania, Revocatus alimpongeza mwekezaji huyo na kumhakikishia kwamba serikali inaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji ili kuwawezesha kukuza biashara zao.

Alisema vikwazo vyote vya biashara vimefanyiwa kazi kimoja baada ya kingine na lengo ni kuendelea kuwavutia wawekezaji wa nje na wa ndani ya nchi waweze kuchangamkia fursa za uwekezaji.

"Serikali inahamasisha wawekezaji wa ndani kama wewe na iko kwenye kampeni ya kuwahamasisha wengine wajisajili TIC kwaajili ya miradi mbalimbali ya uwekezaji ili nao wanufaike na rasilimali za nchi kwa kukuza vipato vyao na vya familia zao," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tanfeed, Faustin Lekule, aliipongeza TIC kwa kutembelea wafanyabiashara mikoani ili kuleta hamasa kwa Watanzania wengi kusajili miradi yao kwenye kituo hicho na kutumia fursa za uwekezaji.

"Kuna faida nyingi kwa mwekezaji kujisajili TIC na sisi ni mashuhuda wa hili kwasababu wametusaidia kuingiza vifaa na mitambo ambayo tunatumia sasa hivi kwa hiyo natoa wito kwa watanzania wanaotaka kuwekeza waende TIC watapata taarifa sahihi na faida nyingi kwenye uwekezaji wao," alisema.

## HABARI PICHANI

# MAANDAMANO YA AMANI YA CHADEMA KATIKA PICHA



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Taifa, Freeman Mbowe, Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Tundu Lissu na Katibu Mkuu, John Mnyika wakihitimisha maandamano ya amani katika Ofsi za Umoja wa Mataifa (UN) Sinza, Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**



Makamu Mwenyekiti wa Chadema Taifa, Tundu Lissu na Katibu Mkuu wa chama hicho, John Mnyika wakiongoza maandamano yaliyoanzia eneo la Mbezi Mwisho jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**




Wanachama wa Chadema wakiwa kwenye maandamano yaliyoanzia Mbezi Mwisho, jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**




Mwenyekiti wa Chadema Taifa, Freeman Mbowe, Joseph Mbilinyi " Sugu" na Godbless Lema wakishiriki maandamano hayo. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Waendesha Bodaboda wakishiriki maandamano hayo. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Walinzi wa chama hicho, wakimdhibiti mtu aliyetaka kumvamia Mwenyekiti wa chama wakati wa maandamano hayo. **PICHA: JUMANNE JUMA**



## HABARI KANDA YA ZIWA

# Kaya 1,600 zanyemelewa na ugonjwa kipindupindu

**Na Waandishi Wetu**

KAYA 1609 katika Kata mbalimbali za Mkoa wa Shinyanga, zimetajwa kutokuwa na vyoo huku wakazi wake wakilazimika kujisaidia vichakani hali inayosababisha ugonjwa wa kipindupindu kuendelea kuwa tishio katika maeneo hayo.

Takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 zinaonyesha kata ya Kinaga iliyoko manispaa ya Kahama, ina Kaya 758 ambazo hazina vyoo kabisa ikifuatiwa na Iyenze yenye Kaya 604, Nyahanga 105 na 142 Kata ya Idukilo wilayani Kishapu.

Mrasimu wa Ramani kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Nolasco John, alitoa takwimu hizo wakati wa mafunzo ya usambazaji wa matumizi ya matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 kwa viongozi na makundi mbalimbali ya Mkoa wa Shinyanga na kuitaja kata ya Kahama mjini kuongoza kuwa na vyoo bora.

Mwakilishi wa Mtakwimu Mkuu wa Serikali Benedict Mgambi alisema, ni wakati wa watendaji wa serikali kutumia takwimu za sensa katika kuwahudumia na kufikisha maendeleo kwenye jamii na kwa takwimu za ukosefu wa vyoo zilizotolewa wahusika wafikiwe na kuelimishwa juu ya umuhimu wake.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, alithibitisha jana alipotembelea kata ya Idukilo yenye visa 132 kuwa mkoa huo una vifo sita vilivyotokana na kipindupindu huku wagonjwa wakifikia 139 pamoja na 398 waliokutwa na wagonjwa hao.

"Wananchi wanapojisaidia vichakani hasa katika msimu huu wa mvua, kinyesi hurudi kwenye vyanzo vya maji, na maji hayo ndiyo wanayatumia na kusababisha ugonjwa kuendelea kuwepo. Hapa tu Idukilo, wanawake 80 wameathirika na ugonjwa wa kipindupindu na wanaume wakiwa ni 59 hali inayoifanya wilaya hii kuongoza kwa ugonjwa huu," alisema.

Mndeme alisema ni aibu kwa kaya zote hizo kutokuwa na vyoo na tayari yalishatolewa maelekezo ili zijenge vyoo na juzi ilikuwa mwisho, hivyo kuwaagiza wakuu wa wilaya kuanza msako kubaini kaya zisizo na vyoo ili zichukuliwe hatua ikiwamo kutozwa faini na zile zinazoshindwa kufikishwa mahakamani.

Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Tumaini Nagu, aliwataka wananchi kuzingatia usafi wa mazingira muda wote pamoja na kunawa mikono kwa majisafi na salama na sabuni wakati wa kula vyakula na kuacha kufua nguo kwenye vyanzo vya maji.

Aliwataka pia wananchi pale wanapomwona mtu ana tatizo la kutapika na kuhara wamwahishe kwenye huduma za afya ili apate matibabu.

**Imeandaliwa na Marco Maduhu (KISHAPU), Shaban Njia (KAHAMA).**



Mratibu wa Chanjo wa Kituo cha Afya Buzuruga, Damaris Dauson, akimpima uzito mtoto, kwenye kliniki ya watoto kituoni hapo, wilayani Ilemela, Mkoa wa Mwanza jana. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Jiji Mwanza lajivunia mafanikio shule ya mchepuo wa kiingereza

**Na Vitus Audax,** MWANZA

HALMASHAURI ya Jiji la Mwanza imejivunia mafanikio ya Shule ya Msingi Nyanza yenye mchepuo wa Kiingereza iliyoanzishwa kwa ajili ya kuinua kiwango cha ufaulu jijini hapa.

Mafanikio hayo ni kuendelea kila mwaka kupanda kwa ufaulu na kuongeza idadi ya wanafunzi wanaosajiliwa.

Akiwasilisha utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa Kata ya Mirongo 2020- 2025 jana, Diwani wa Kata hiyo ambayo shule hiyo ipo, Hamidu Suleiman, alisema kwa mwaka huu, usajili umeongezeka kutoka wanafunzi 90 hadi 150.

Suleiman alisema mpaka kufikia mwishoni mwa wiki iliyopita, shule hiyo ilikuwa tayari imesajili wanafunzi wa awali 150 zaidi ya makadirio ya kusajili wanafunzi 100 kwa mwaka huu huku darasa la kwanza ikisajili wanafunzi 250 mara mbili ya mwaka jana.

"Lengo la kuanzisha shule hii ilikuwa kuhakikisha Halmashauri inapunguza au kuondoa kabisa ziro ikiwa ni pamoja na kuinua kiwango cha ufaulu kupitia shule hii ya mfano," alisema Suleiman.

Pia alisema halmashauri imeamua kupinguza ada katika shule hiyo kutoka Sh.600,000 kwa mwaka hadi Sh.400,000 lengo likiwa ni kuhakikisha hadi mwananchi wenye uwezo wa kawaidi kumudu.

Diwani huyo alitaja mafanikio mengine kuwa ni pamoja na ukarabati wa miundombinu ya barabara ulioambatana na kuweka taa 91 za barabarani, maboresho ya Shule ya Sekondari ya Mirongo ambayo imeongezewa jengo la ghorofa huku wakiendelea na utaratibu wa kujenga vyoo shuleni hapo.

Vilevile alitaja ujenzi wa soko la Mirongo kuendelea vyema na kuwa mpaka sasa umefikia asilimia 80 huku likitarajiwa kuendelea kuwahudumia wafanyabiashara wa ndani na nje ya jiji hili kutokana na kuwa maaru kwa biashara ya Matunda.

Ofisa Elimu wa Kata ya Mirongo, Grace Mwanjonde, aliwakumbusha wazazi ambao hawajapeleka wanafunzi kuandikishwa awali, darasa la kwanza pamoja na kuripoti kidato cha kwanza, kuhakikisha wanafanya hivyo haraka iwezekanavyo kwa kuwa serikali haitowavumilia.

"Pelekeni watoto shule hata kama hawan sare anatakiwa akaripoti kwani tayari masomo yameanza hivyo kuweni mabalozi kwa wengine kwani serikali haipo tayari kuwavumilia wanaowaficha wanafunzi,"alisema Mwanjonde.

## Ulega ataka ranchi kuvutia uwekezaji

**Na Jenesta Jasson,** BUKOBA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amewaagiza viongozi na wataalamu wa Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) mkoani Kagera kufuatilia ranchi zote mkoani hapa kubaini zilizo wazi kisha kuzitangaza kwa ajili ya uwekezaji.

Alibainisha ranchi hizo kuwa ni Kagoma iliyoko wilayani Karagwe na Mwisa II wilayani Muleba pamoja na wilayani Karagwe na kuwataka kufanya ufuatiliaji wa kina na kubaini kama maeneo hayo hayana changamoto yoyote yatangazwe ili kuliongezea taifa mapato.

Waziri Ulega alitoa agizo hilo juzi katika mkutano na viongozi wa mkoani hapa kwa lengo la kutatua baadhi ya migogoro inayoendelea katika ranchi hizo zinazohusisha wananchi waliokuwa na makazi yao kwenye ranchi hizo.

"Kazi hii isichukue muda mrefu ili kuruhusu watu kuwekeza katika maeneo hayo na wawekezaji wafanyiwe tathmini kuepukana na kuwapa wababaishaji ili nchi ipate manufaa na kuwanufaisha wananchi pia," alisema Ulega.

Mkuu wa Wilaya Bukoba, Erasto Sima, aliahidi kushirikiana na viongozi wenzake na wataalamu ili kutatua migogoro iliyoko kwenye ranchi ikiwa ni pamoja na kuruhusu wawekezaji.

Naibu Katibu Mkuu, Sekta ya Mifugo, Daniel Mushi, alisema utaratibu wa kukamilisha ranchi hizo kwa ajili ya wawekezaji zinaendelea hasa kwa ranchi ya Mwisa II inayopita wilaya za Mleba na Karagwe. Alisema kati ya vitalu 52 vilivyoko Muleba, saba tayari amepewa mwekezaji na 11 vimetolewa kwa halmashauri.

Alisema wamekubaliana na NARCO kwa ajili ya kutafuta wawekezaji kwa kuwa vitalu 34 viko tayari kwa ajili ya uwekezaji na kuahidi kutekeleza maelekezo ya Waziri ipasavyo.

# ama

ALHAMISI JANUARI 25, 2024

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Dawa kulevya zinavyomletea uraibu mtoto tangu tumboni kwa mama**



Ukurasa 13

Sura kamili nyama ya kuku wa kizungu na salamu za usiyoyajua



Ukurasa 14

**Mradi unaowapatia maisha mapya wenye VVU kiafya, elimu, hadi mlo**

WIKI SABA ZENYE MAGEUZI GHAFLA...

# Mafuriko yalivyowafikia Katesh na Rais alivyowaandalia maisha mapya

**Na Halfani Chusi**

- Wahisani 434 wamuunga mkono na Bn. 3.17/-
- Alianzia Ngorongoro, maisha mapya mabadiliko

ALFAJIRI ya Desemba 3 ya mwaka jana ilianza vibaya kwa wakazi wa wilaya ya Hanang mkoani Manyara, wakazi wakikumbwa na maafa ya maporomoko ya tope yaliyoandamana na miamba, mawe, magogo, na mabaki ya nyumba zilizokuwa zikizolewa na hatimaye kuathiri vitongoji.

Hilo likawa pigo kwa vijiji na kata zilizopo kando ya mlima Hanang na kata nne za mji mdogo wa Katesh. Ni maafa ambayo jumla ya watu 89 walipoteza maisha na wengine 139 kujeruhiwa.

Waliopoteza nyumba au kuharibikiwa wako 1,292. Hivyo, serikali ikagharamia mazishi na kutoa mkono wa pole kwa kila mwili uliopatikana, pia kugharamia matibabu ya waathirika wote.

Ni mkasa uliomfanya Rais Dk.Samia Suluhu Hassan, kukatiza safari aliyokuwa kikaoni nje ya nchi, kisha akarejea kuungana ana baadhi ya mawaziri walioongozwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kwa hatua za nusura na huduma kuchukuliwa kwa waliofikwa.

Mengi yalitimizwa yakioongozwa na maelekezo ya Rais Dk. Samia, yakiendana na kufungua kambi tatu za kuhifadhi waathirika 534, huku wengine 156 waliofika asubuhi na kuondoka jioni.

Wakanufaika kwa hatua za matunzo, chakula, malazi, matibabu, usalama na hali ilipotulia, wakasaidiwa kuungana na ndugu na jamaa zao. Jumla yao 690 walifanikiwa kurejea kwenye jamii.



Hali ilivyokuwa katika mafuriko ya Katesh, wilayani Hanang. **PICHA: MTANDAO**

**MSEMAJI SERIKALI**

Msemaji wa Serikali, Mobhare Matinyi, analifafanua hilo kwamba, kuna jumla ya askari 1,285 kutoka majeshi na vikosi mbalimbali walishiriki kuwaokoa waathirika

“Serikali pia ilipokea misaada ya chakula cha aina mbalimbali na vitu muhimu kwa mahitaji ya kila siku kama nguo, viatu, mashuka, blanketi, magodoro, majiko ya gesi na mitungi yake, vyombo vya jikoni.

“Hadi kufikia sasa misaada hii imefikia thamani ya Sh. Bilioni 3,174,655,188.00. imetoka kwa wahisani 443, ambao ni watu binafsi, asasi, kampuni, mashirika, taasisi binafsi na za umma, vyama vya siasa, taasisi za dini na za kimataifa.

“Serikali pia ilikusanya fedha za misaada kupitia akaunti ya Mfuko wa Taifa wa Misaada ya Maafa iliyoko Benki Kuu ya Tanzania. Fedha hizo zimefikia jumla ya shilingi bilioni 2.7.

“Pamoja na zile Sh. bilioni 2.5 zilizoletwa na Rais Samia Suluhu Hassan, kiasi kinachokamlisha jumla ya fedha zote kufikia shilingi bilioni 5.2,” anasema Matinyi, ambaye pia ni Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo

Anafafanua kwamba, kwa sasa serikali imeanza kutekeleza ahadi ya kuwajengea waathirika nyumba 101, zitakazojumuisha nyumba 89 zilizothibitika kubomoka baada ya maafa hayo na zingine 12 ambazo wataalam wa serikali wameshauri zibomolewe na eneo lake lisitumike kwa makazi au shughuli zozote kiuchumi na kijamii.

Mantinyo obhare anasema, katika hilo serikali imetenga ekari 100 za kujenga makazi mbadala, katika shamba la Waret, lililopo kwenye eneo la Jeshi la Magereza, kwenye kijiji cha Gidagamowd, kata ya Mogitu, wilayani Hanang.

Ni eneo lililoko kilomita 4.5 kutoka Barabara Kuu ya Babati-Singida na kilomita 21.2 kutoka mji mdogo wa Katesh, kuelekea Singida.

Anabainisha kazi zilizokamilika hadi sasa, ni upimaji viwanja na usajili wa ramani ya eneo la ujenzi, kukiwapo viwanja 269 vilivyopimwa, kati yake 226 ni makazi.

Mengine anataja ni viwanja 26 vya makazi na biashara; 17 huduma za kijamii kama zahanati, maziko, kiwanja cha michezo na eneo moja la wazi; viwanja vya ibada vitatu; ofisi ya kitongoji, soko na shule ya msingi.

“Hatua inayofuata ni umilikishaji viwanja kwa waathirika, ukamilishaji ubunifu wa ramani za nyumba, gharama na zijengwe na nani, lakini mpango ni kufanya kazi kwa mtindo wa opereshени kwa muda wa miezi mitatu,” anafafanua.

Kuhusu kutathimini hasara ya mashamba, Mantinyi anasema kuna ekari 755 mashamba ya wakulima, kati yake 369 zilishaharibiwa.

Anafafanua katika kuwafuta machozi, serikali imegawa mbe-


**INAENDELEA UK. 13**

AFYA

# Dawa kulevya zinavyomletea uraibu mtoto tangu tumboni kwa mama

**Na Zanura Mollel**

• Yajue yanayomkuta mama, baba yake



XXX. **PICHA: MAKTABA**

KUNA hoja inayojirejea mara zote na kimsingi haifi, nini maana ya dawa za kulevya? Kitaalamu inatafsiriwa ni "kemikali ambazo zikiingia mwilini, huathiri ubongo wa mtumiaji na kumsababishia kuwa na matendo, hisia, fikra na muonekano tofauti na matarajio ya jamii.'

Mzizi wa dawa hizo unatajwa ni kemikali zitokanazo na mimea na madini, ambazo ni malighafi muhimu kwa mahitaji mengine ya mwanadamu. Dawa hizo huingia mwilini kwa njia kuu tatu; kunywa, kula na kujidunga sindano

Kisheria zipo dawa zilizoruhusiwa kama tumbaku na pombe na zisizoruhusiwa kama bangi, mirungi, kokeini, heroin na mandrax; na zinazoruhusiwa kutumika hospitali kama valium, pethidine na morphine.

**RIPOTI MWAKA 2022**

Ripoti inayotolewa na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) kwa mwaka 2022, inaonyesha idadi ya waraibu waliosajiliwa kwenye Huduma ya Tiba Saidizi (MAT) ilikuwa 13,696 katika mchanganuo; wanaume 13,089 na wanawake 607.

Vilevile, waliopata huduma katika nyumba za upataji nafuu (sober house) ilikuwa 3,180; wanaume 3,056 na wanawake 124.

Kupunguza madhara ya dawa za kulevya, serikali imeendelea kuboresha matibabu kwa waraibu wa dawa hizo, mwaka 2022 walikuwapo waraibu 854,134; wanaume 434,847 na wanawake 419,287 waliopatiwa huduma katika vituo vya afya ya akili nchini.

**RIPOTI 2023**

Ripoti ya Dunia ya Dawa za Kulevya mwaka jana, iliyozinduliwa na Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kupambana na Dawa za Kulevya na Uhalifu (UNODC) inasema, kuendelea ongezeko la usambazaji haramu wa dawa za kulevya, kunakozidisha changamoto za huduma za afya na utekelezaji sheria hiyo.

Pia, kunatajwa idadi ya wanaougua matatizo hayo, imeongezeka kufika watu milioni 39.5, ni ongezeko la asilimia 45 katika kipindi cha miaka 10.

Vijana wanatajwa kuwa hatarini zaidi, pia ndio wanaoathiriwa zaidi katika maeneo tofauti duniani, ripoti ikiangaza:"Barani Afrika, asilimia 70 ya w matibabu dhidi ya dawa za kulevya wako chini ya umri wa miaka 35".

Duniani, kunatajwa kuwapo watu milioni 296 wananatumia dawa za kulevya na kwa kipindi cha maka 10 kufika 2021, kulikuwapo ongezeko la asilimia 23.

> **Dawa hii ipo katika mfumo wa kimiminika, hutolewa kwa kipimo. Ukikosea kipimo, unaweza kusababisha kifo kwa mtumiaji, matibabu kwa waraibu inachukua miaka miwili.**

Pia, takwimu mpya zinakadiria mwaka 2021 kimataifa, kumekuwapo watu milioni 13.2 wanaojidunga sindano za dawa za kulevya, ikiwa ongezeko la asilimia 18 miaka kabla ya hapo.

Ripoti inashauri kipaumbele kwa afya ya umma duniani kote, pia kinga na kufikia huduma za matibabu, vinginevyo kasi ya kuenea dawa za kulevya itazidi.

Athari inaanzia kiitwacho kitaalamu 'Asidi Deoksiribo Nukleini(ADN au DNA) hubeba vinasaba (genes), kwa maana ya sehemu zinazoamua tabia za kiumbe husika kama vile mwonekano, jinsia na kilichopokea kutoka wazazi wake.

Wanyama, mimea, bakteria na virus, wote wana 'DNA Molekuli' inayobeba ndani yake habari zote za urithi wa kiumbehai husika; taafrifa za tabia zinazopokewa kutoka kwa wazazi. Zimo 'jeni' zinazotunza habari maalumu juu ya urithi wa kiumbe.

DNA ina uwezo wa kujinakiri wakati wa kuzaa, ikijipasua katika pande mbili, Upande wa mzazi mmoja inaungana na mzazi mwingine.

Tabia kama za ukubwa wa mwili, rangi ya ngozi au nywele, zote ziko kila moja mahali pake; zikiunganishwa za baba na mama.

Kemia inaamua ni upande wenye athari zaidi, hivyo inajitokeza kwa mtoto wakitaja kwa jina "DNA inatokea ndani ya kinachoitwa 'kromosomu' na 'kiini cha seli".

**DNA NA DAWA**

Kumekuwapo taarifa za athari za dawa za kulevya kiafya, ikiwamo uhusiano wa mjamzito anayetumia, hata akajifungua mtoto mwenye chembe za uraibu.

Mkuu wa Idara ya Afya ya Akili Hospitali ya Rufani Mkoa wa Arusha Mount Meru, Dk Salum Said, ambaye pia ni Msimamizi wa Kitengo cha Huduma ya Methadone, anasema kuna uhusiano mkubwa wa mtoto kuzaliwa na vimelea vya uraibu, mzazi anapotumia dawa za kulevya.

Anafafanua kuwapo athari zaidi kupitia kwa mjamzito, kutokana na mtoto tumboni anakula kwa kutumia kitovu cha mama yake (placenta), hata kabla hajazaliwa.

"Chochote anachokula mama na mtoto anapokea, dawa za kulevya zinakwenda moja kwa moja kwenye ubongo wa mtoto," anasema Dk. Said.

Anaeleza kuwa, mtoto tajwa anapozaliwa,, anakuwa na dalili za uraibu, sababu ni kukosa vichangamshi, hivyo asiponyonyeshwa, hulia sana, anapata degedege, anatetemeka, hata kupiga miayo mingi.

Mtalamu huyo wa dawa za kulevya anashauri: "Tunawazingatia wanapokuwa wajawazito kujifungulia katika kituo cha afya kwa ajili ya uangalizi zaidi."

**WANAUME JE?**

Dk. Said anasema kinababa, athari zao ni kukosa nguvu za kiume, kutoshiriki tendo la ndoa kwa muda mrefu na anashindwa kufikia mshindo(kileleni), wengine wanaiishia mshindo mmoja pekee.

"Watu wenye umri wa miaka 25 hadi 40 wanatajwa kuwa waraibu wanaopata matibabu katika hospitali hiyo, huku asilimia 90 wakiwa ni wanaume. Hata hivyo, kati ya watu wanne hadi watatu wanaotumia dawa za kulevya, mmoja anaweza kuibuka kuwa mraibu," anafafanua Dk. Said.

**MAGONJWA YANAYOWAPATA**

Dk Said, anasema asilimia 64 ya waraibu wanaopata matibabu hospitalini hapo, wamebainika kuwa na maambukizi ya ugonjwa wa Homa ya Ini C.

Aidha, anataja kuwapo ongezeko kubwa la wenye maambukizi ya Virusi vya UKIMWI, sampuli za waraibu zikionyesha zaidi kwa asilimia 10, inachangiwa na sindano wanapojidunga dawa za Heroin.

Vilevile anataja waraibu wa pombe, wanaposhiriki tendo la ndoa bila ya kutumia kondomu, akinena wanaishia kupata maambukizi ya VVU, kutokana na kushiriki tendo hilo wamelewa na hawakumbuki matumizi ya kondomu, hata kuishia maambukizi ya UKIMWI."

**NAMNA WANAVYOTIBIWA**

Kitengo cha Methadone kwa waraibu wa mkoani Arusha chenye miaka miwili tangu kuanzishwa, imeshahudumia waraibu 700 na Dk Said anaeleza matibabu yao ni bure, dawa hizo kuwa chini ya uangalizi maalum na mraibu analazimka kutumia akiwa hospitalini.

"Dawa hii ipo katika mfumo wa kimiminika, hutolewa kwa kipimo. Ukikosea kipimo, unaweza kusababisha kifo kwa mtumiaji, matibabu kwa waraibu inachukua miaka miwili," anasema Dk Said.

Anafafanua tiba dawa ya dawa za methadone ina inajumuisha mengi, ikiwamo majipu kwa mraibu, kutokana na kujidunga sindano, kufubaza VVU, Homa ya Ini na Kifua Kikuu.

"Kuna kitengo cha ustawi wa jamii kwa lengo la kuwakutanisha wale waliotengwa na familia zao kutokana na uraibu pamoja na kitengo cha saikolojia kinachowalea kwa kuwashauri mambo mbalimbali," anasema Dk. Said.

AFYA

# Sura kamili nyama ya kuku wa kizungu na salamu za usiyoyajua

**Na Mwandishi Wetu**

HIVI sasa wafugaji wengi hutegemea zaidi kuku kizungu wakiitwa 'kuku wa kisasa.' Kwa vyovyote vile, kula kile unachozalisha nyumbani ni bora kuliko kuku waliogandishwa kutoka nje," anaamini Eugène, mjasiriamali wa nchini Mali.

Anaendelea: "Kwa sababu unapoweka kuku wa kienyeji au wa asili sokoni, watu wanawaona kuwa ni wa gharama sana ingawa ni kuku wenye afya zaidi na wana virutubisho muhimu zaidi kwa mwili."

Kwa ujumla, wataalamu wa lishe wanapendekeza ulaji wa nyama nyeupe kwa faida nyingi zilizomo kiafya. Kuku wa kienyeji wanapendekezwa zaidi, hata kuwa chakula adimu, kwani wafugaji hupata faida zaidi katika ufugaji wa kuku wa nyama.

Eugene anadokeza kwamba, kukuza inachukua siku 21 kwa yai la kuku wa nyama kukomaa kuwa kifaranga, ambacho kitakuwa tayari kuliwa ndani ya miezi mitatu pekee.

"Hapa katika soko la Gbossimé (nchini Togo), kuku wa kienyeji wanauzwa 4,500 FCFA (fedha zao), huku wale wa nyama wakigharimu 3,500 FCFA. Unaweza kuona tofauti kidogo. Ni wazi kwamba tunaweza kumudu kununua tu kile ambacho ni cha bei nafuu, kutokana na matatizo ya sasa ya kifedha," Mama Kayi, mama wa nyumbani.

Hata hivyo, mtaalamu wa lishe, usafi na ubora wa chakula, Dk. Matthieu Tobossi, anasema kuku wa kisasa wanafaa kuliwa kiasi kidogo, ikizingatiwa kwa msingi ni viumbe vilivyobadilishwa vinasaba.



Nyama ya kuku waliokwishaandaliwa. **PICHA ZOTE: MAKTABA**

### INAVYOLISHA UMMA

Kuku wa kisasa wanatajwa wanazalishwa haraka na kwa wingi ili kukidhi mahitaji ya mlo kijamii duniani, migahawa na hoteli inayowahitaji zaidi.

"Hivyo, hatuwezi kutarajia kuku wa kienyeji au wa asili katika kiwango hiki. Kuku wa nyama hukidhi vyema mahitaji haya. Tunajaribu kupunguza usambazaji wa kemikali kwa kuku hawa kwa njia bora iwezekanavyo," anasema Koffi G, mfugaji mwingine nchini Togo.

Anasema kuku hao wanaofugwa kwa uzalishaji nyama, pia huitwa 'gril', wakiwapa walaji virutubisho kulingana na wataalamu wa lishe, akitaja kuwa chanzo muhimu cha lishe kwa umma.

Maangalizo ya wataalamu lishe ni kwamba, mara nyingi yanaonyesha kuwa kuku kwa ujumla, ni pamoja na nyama, yakiwa na vitamini nyingi na vitu vingine vingi vinavyotoa thamani kubwa ya lishe kwa mwili wa binadamu.

Anavitaja, ni zaidi ya kemikali zinazodungwa kwenye kuku wa nyama kuwafanya waweze kuliwa haraka, pia wana vitu vya kuvutia kama kuku wengine.

Kuku hao wa kisasa mara nyingi hulishwa ngano, mahindi, protini, vitamini na kufuatiliwa kiafya. Asidi muhimu za mafuta, pia inatajwa kuwa sehemu ya lishe zinazochangia thamani ya lishe ya nyama ya kuku wa kisasa kwa mwili wa binadamu, kwa mujibu wa Dk Tobossi.

### NYAMA NA PROTINI

Kuku wa nyama wanatajwa kuwa na protini zinazochangia ukuaji wa misuli yao. Inatajwa seli zote za tishu zilizo hai, na protini ni muhimu kwa utendaji mzuri wa mwili wa mwanadamu.

Katika nafasi yake wataalamu hao wanasema kuku wa nyama huwa na protini zinazochangia ukuaji misuli. Kula kuku kunatajwa ni muhimu kwa misuli, mifupa yake na homoni, kulingana na wataalamu wa lishe.

Wanasema nyama ya kuku hutoa asidi za amino ambazo mwili hauwezi kuizalisha, bali ni kupitia chakula na hasa kuku. Asidi hizo wanazitaja ni muhimu mwilini kwa mlaji. Kutokana na lishe yake, kuku hao wanatajwa kuwa na vitamini nyingi, nyama zao zinatoa vitamini B3 inayoitwa niasini. Ni vitamini inayosaidia kuweka ngozi kuwa na afya. Pia, kuna vitamini B6 ambayo inashiriki katika mchakato wa udhibiti na ujenzi wa tishu kutoka kwa protini.

Kuku pia wanazo vitamini B5 au asidi ya pantothenic, muhimu kwa kuifanya ngozi na nywele kuwa mpya. Pia, inasaidia utendaji mzuri wa mfumo wa kinga mwilini.

Wataalamu wa lishe wanapendekeza, ulaji nyama ya kuku zaidi kuliko ngozi, maana gramu 100 ya nyama ya kuku hutoa zaidi ya asimilia 50 ya lishe ya kila siku.

Hizo ni kalori, vitamini na madini inayotolewa mwilini. Dk Toboss anawataja kuku, kwa jina 'chakula cha wajenzi', akinena "inapendekezwa kwa watoto, wazee, wajawazito, wanamichezo, wagonjwa.... "

### ULINGO WA TAHADHARI

Wafugaji wengi wanatajwa kutumia kemikali na homoni za ukuaji na kwa hiyo matumizi yake ya mara kwa mara yanaweza kusababisha matatizo ya kiafya, kwa mujibu wa wataalamu wa lishe wanaodai kuwa ni kwa sababu ya kemikali zinazotumika kwa ukuaji wa haraka wa kuku hawa.

"Tuligundua kuwa baadhi ya wafugaji hutumia kupita kiasi dawa za antibiaotiki kwa kuku kupita kiasi. Hii husababisha bakteria wa matumbo na straphylococci kuongezeka," anasema Dk Tobossi, anayesisitiza ndio chanzo cha magonjwa ya moyo na mishipa na kudhoofika kwa mfumo wa kinga.

Anasema nyama hiyo inabaki na chembe chembe nyingine za kemikali ambazo ni hatari, hasa maradhi ya moyo. Pia, kuku wa nyama wengi wanafugwa katika mazingira ambayo sio ya asili kwa ndege, hata inapunguza ubora wa nyama yao.

**• Kwa mujibu wa BBC.**

## Mafuriko yalivyowafikia Katesh na Rais alivyowaandalia maisha mapya

**INATOKA UK.12**

Anafafanua katika kuwafuta machozi, serikali imegawa mbegu za kupanda shilingi milioni 33, ambazo ni za alizeti, mahindi, ngano na maharage,akiaahidi mgawo wa mbolea kwa wakulima 371 wahitaji.

### HALI YA MIFUGO

Kuhusu mifugo iliyoathirika, Matinyi anasema inawagusa wafugaji 23 waliopoteza mifugo, thamani yake inakadiriwa Sh. milioni 64.9, mgawanyiko wake ukiwa; ng'ombe 70, mbuzi 115, kondoo 102, nguruwe 12, sungura 15 na kuku 264.

Anasema kwa sasa kuna wateja 376 waliokwisharejeshewa huduma za umeme, pia mawasiliano mengine, sambamba na juhudi za kuokoa na kuopoa.

### KUHUSU NGORONGORO

Kuhusu hifadhini Ngorongoro, ambako kuna maelekezo ya mkuu wa nchi- Dk Samia, mhusika anasema wananchi wanahama kwa hiari kutoka wanakoishi hifadhini Ngorongoro, akitaja hadi katikati ya mwezi huu, kaya 30 zenye watu 224 na mifugo 393, zilishahamia kijijini Msomera.

Analitaja hilo ni kundi la kwanza katika awamu ya pili ya wananchi wanaohamia Msomera, kuungana na wananchi 3,010 watokanao na kaya 551 na mifugo 25,521 waliotangulia awamu ya kwanza, baada ya nyumba zao 503 kukamilika.

"Kundi jingine la kaya 25 zenye watu 172 na mifugo 213 nalo linahama kutoka Ngorongoro kwenda maeneo mengine ya nchi ambayo ni mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Simiyu na Tanga.

"Hili ni kundi la tatu la wanaohamia maeneo mengine. Katika awamu hii ya pili, wananchi wengine waliohamia kwenye maeneo mengine ya nchi nje ya Msomera, ni kaya 27 zenye watu 120 na mifugo 769.

"Hii inafanya jumla ya waliohamia kuwa kaya 52, watu 292 na mifugo 982. Hadi kufikia Desemba 31, mwaka jana tayari nyumba 350 zimeshakamilika kijijini Msomera. Hivyo basi, zoezi la kuhama litaendelea kwa mwezi huu wote wa Januari 2024," anatamka

Mosi, Mantinyi anataja ni kuwahamishia wananchi wa Ngorongoro kwenye eneo bora zaidi kwa maendeleo yao ya huduma za kijamii, vilevile usalama wao.

Pili, anasema ni hatua inayopendeza na kutunza uhifadhi wa Ngorongoro, eneo linaloheshimika kimataifa, kuwa urithi wa dunia.

"Kwa kila mwananchi anayehamia kijijini Msomera, anamilikishwa nyumba ya kisasa yenye vyumba vitatu katika eneo la ekari 2.5, pamoja shamba la ekari tano.

"Mwananchi huyo mbali ya kulipwa fidia ya mali zake alizoacha Ngorongoro kama makazi na mazizi, anaongezewa pia shilingi milioni 10 na atasafirishwa yeye na familia yake na mali zake zote, ikiwamo mifugo hadi Msomera au eneo jingine atakalolichagua.

AFYA

HEBU TUYAJENGE

# Mradi unaowapatia maisha mapya wenye VVU kiafya, elimu, hadi mlo

**Na Beatrice Philemon**

INAWEZEKANA ikizungumziwa mradi wa Hebu Tuyajenge, siyo Watanzania wengi wanaufahamu, hata hivyo ina yake makubwa kwa wananchi.

Ni mradi ulioanzishwa mkoani Iringa kusaidia watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi wapate tiba na lishe bora, ili kujikwamua kiuchumi. Pia unaazimia kuongeza upimaji, hata uzazi wa mpango.

Mradi Hebu Tuyajenge, huwashirikisha Watu Wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (WAVIU) kupitia Baraza la Taifa la Watu Wanaoishi na VVU Tanzania (NACOPHA) .

Pia, unawalenga vijana wa umri balehe, kuongezeka katika upimaji VVU, tiba na uzazi wa mpango, ili kuimarisha mazingira wezeshi ya mwitikio wa vita dhidi ya UKIMWI kupitia kundi hilo.

Mkoani Iringa, mradi umepata ufadhili wa Mpango wa Dharura wa Rais wa Marekani wa Kukabiliana na UKIMWI (PEPFAR), kwa kushirikiana na Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID).



Wanufaika wa mradi Hebu Tuyajenge, katika matukio yao tofauti. **PICHA: MAKTABA**

### KUNUFAIKA NA MRADI

Akizungumza na Nipashe, Katibu wa Kikundi cha Itika, chenye wanachama wanaoishi na Virusi Vya Ukimwi katika Manispaa ya Iringa, Akiba Lwisa, anasema kikundi chao ni kati ya orodha 32 ya vikundi vyenye wanachama 491 wanaoishi virusi hivyo na wamenufaika na mradi Hebu Tuyajenge.

Lwisa anasimulia safari yao kunufaika na mradi, ilianza mwaka 2021 wafanyakazi kutoka NACOPHA walipokifikia kikundi chao kuwaelimisha, namna sahihi ya matumizi ya dawa za kufubaza VVU, kuwapa mafunzo ya kujiwezesha kiuchumi.

Hapo anasema ikagusa, kuweka akiba na kukopeshana kwa riba nafuu, kuwahamasisha kila mwanachama kuwa na bima ya afya iliyoboreshwa na kuwawezesha kufuatilia hali halisi kwenye kaya masikini kuhusu lishe bora.

Pia, akatamka wamepata vifaa vya kutengeneza mikate ikiwa ni sehemu ya nyenzo ya uzalishaji, yenye thamani ya shilingi milioni mbili kutoka PEPFAR.

Kupitia elimu waliyoipata hadi sasa, anasema kikundi kimeanzisha kiwanda cha kutengeneza mikate kilichopo kata ya Mwangata, Manispaa ya Iringa, ikiwaongezea kipato, pia kuwapa lishe bora , kusomesha watoto wao na kuwarahisishia huduma bora za afya,

> **Tayari tumeanza kutengeneza mikate ya aina mbalimbali na uzalishaji wa mikate umeongezeka kutoka mfuko mmoja wa unga wa ngano wenye kilogramu 25 hadi mifuko mitatu ya unga wa ngano kwa siku.**

"Tayari tumeanza kutengeneza mikate ya aina mbalimbali na uzalishaji wa mikate umeongezeka kutoka mfuko mmoja wa unga wa ngano wenye kilogramu 25 hadi mifuko mitatu ya unga wa ngano kwa siku," anasema.

Fedha waliyoipata, Lwisa anasema imewafanikisha kupunguza deni la mkopo kutoka Halmashauri ya Manispaa Iringa, wamelipa pango la nyumba, wameweka akiba ya shilingi 700,000, kwenye akaunti ya kikundi na hadi sasa kuna shilingi 650,000 zimetolewa kukopesha wanakikundi waanzishe biashara zao binafsi.

Anataja miradi ya wanachama ya kujiongezea kipato kama vile utengenezaji wa batiki, kilimo cha mboga na matunda, ushonaji, ufugaji na kuweka na kukopa.

Pia fedha nyingine, anasema wanatumia kuongeza kwenye mtaji, pia wanaweka hisa na kukopeshana kwa riba nafuu, ili kuwasaidia wanakikundi kiuchumi.

Anafafanua, kuna wanachama 14 wamepata kadi ya bima ya afya, wengine wanasomesha watoto wao kupitia faida ya kuuza mikate, akijivuna maisha ya wanachama yameimarika, kipato chao kuongezeka.

Kwa mujibu wa katibu huyo, hivi sasa wanakula milo mitatu, tofauti na miaka ya nyuma, siri kuu ikiwa biashara ya mikate waliyo nayo.

"Kabla ya mradi, watu walikuwa wanakula mlo mmoja, kutokana na umasikini, lishe ilikuwa duni, watu hawakuwa na miradi ya kujiongezea kipato, uzalishaji wa mazao ya mahindi, alizeti na mazao mengine umepungua, kwa sababu udongo umechoka, hakuna rutuba na mbolea ni gharama," anasema.

Lingine analolitaja Lwisa kusaidiwa na wafadhili NACOPHA, ni jenereta inayowasaidia wakati wa kutengeneza mikate umeme unapokatika ghafla.

"Kwa mteja anayependa kununua mikate yetu, tunauza mikate kijiji cha Itika kilichopo kata ya Mwangata, Manispaa ya Iringa," anasema.

Hivi sasa wanaomba wadau, zikiwamo kampuni binafsi kuwasaidia usafirishaji wa mikate yao, ili wafikie wateja wengi zaidi. Pia, wana wito kujenga kiwanda kikubwa kusaidia wanaoishi na maambukizi ya VVU.

### SAUTI YA NACOPHA

Ofisa Mtendaji wa NACOPHA, Deogratius Rutatwa, anasema mradi wa Hebu Tuyajenge unatekelezwa na NACOPHA katika halmashauri 184, ukigusa eneo la kuboresha maisha ya vijana, mama na watoto, pia kwa maisha ya mtu mmoja mmoja.

Kupitia mradi wa Hebu Tuyajenge, NACOPHA imeshaanzisha vikundi zaidi ya 4000 vya watu wanaoishi na VVU, vikundi hivyo vikichangia kuleta umoja na kupinga unyanyapaa kwa wenye shida hiyo ya kiafya.

Anataja jukumu la vikundi hivyo ni kuwaweka watu pamoja, waelimishane kuhusu VVU, wakipinga vikali unyanyapaa, elimu ya matibabu, kusaidiana katika madhila na kisaikolojia, kupeana elimu rika, kujengeana uwezo, kuleta haki za kijamii, kiafya na tiba.

Rutatwa anasema, hadi sasa NACOPHA ina zaidi ya watoa tiba 2000 wanaofanya kazi kwenye jamii, kuelimisha kuhusu maambukizi ya VVU na tiba yake, wakiwaunganisha wahusika na huduma ziliko.

Anasema kupitia vikundi 4000, watu wanaoishi na VVU wameweza kujiimarisha kiuchumi katika shughuli kama za ujasiriamali, kilimo cha mazao ya chakula, mboga na matunda, biashara kama za ushonaji, kuuza nafaka, kutengeneza mikate na sanaa.

Pia, anafafanua kuna utengenezaji bidhaaa za mikono na hivi sasa, watu wana uwezo wa kujikimu, tofauti na nyuma, kipato chao kiko juu na kupunguza utegemezi kwa ndugu na jamaa, hivyo unawaegua kutoka kwenye unyanyapaa.

Pia, anawaomba viongozi wa dini kuelimisha watu suala la VVU lisionekane kama dhambi, kwani inakuwa katika sura ya 'kuhukumu,' huku akiwasihi watoa huduma nao kuzingatia maadili ya kazi yao, ugonjwa wa mtu ni siri.

Anasema, wao wana- mradi wanazama katika kuhakikisha vikundi wezeshi wanavijengea uwezo kujikimu, kupata huduma za afya, wakiona zao la kupungua unyanyapaa.

Mradi wa Hebu Tuyajenge, husimama katika kushirikisha vikundi vya watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (VVU) katika kubuni, kutekeleza na kufuatilia shughuli za UKIMWI zinazotolewa katika jamiii.

### AFUA ZA MRADI

Afua za mradi ni kutoa elimu ya tiba kwa Virusi vya Ukimwi katika jamii, kutoa elimu ya kuzuia maambukizi mapya miongoni mwa vijana, wakishirikisha viongozi wa imani na jamii katika kuibua wana jamii wenye VVU, kutambua wenza na watoto wao kama wana hali hiyo.

Pia, mradi unatoa usaidizi katika kuzingatia matumizi sahihi ya dawa kwa wahusika kubaki katika matumizi yake; pia wanatoa mafunzo kwa viongozi wa vikundi katika namna ya kuongoza na usimamizi wa fedha, ufuatiliaji wa shughuli za VVU katika jamii, kupambana na kukabiliana na unyanyapaa na ubaguzi wake.





# Mikakati yawekwa kutatua maji UDOM

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeandaa mikakati ya kukabiliana na tatizo la maji katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) chenye wanafunzi 35,000 huku upatikanaji wa huduma ya maji ukiwa wastani wa asilimia 51.

Miongoni mwa mikakati hiyo ni kutengeneza chanzo maalum cha maji cha chuo na kuipa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Dodoma (DUWASA) usimamizi wa upatikanaji wa maji.

Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, akizungumza juzi jijini hapa baada ya kutembelea chuo hicho kukagua upatikanaji wa maji, alisema UDOM inahitaji msaada maalum na kufanyia utafiti wa kina kwenye eneo la chuo lenye maji ili kuchimba visima.

Pia alisema amefuatilia kuna Sh. bilioni moja zilitolewa na serikali lakini amebaini kuna tatizo la uratibu kwa kuwa zilipaswa zipelekwe DUWASA lakini zilipelekwa Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) ambao hawahusiki kwenye usimamizi.

"Tumeamua kuongeza usimamizi na kazi hii tutampa mwenye jukumu la kusimamia kwa sasa mambo yanayohusu upatikanaji wa maji UDOM yatakuwa chini ya DUWASA. Nendeni mkafanye mapitio ya mgawo wa maji ili kuongeza upatikanaji wake," alisema.

Awali, Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Lughano Kusiluka, alisema kutokana na adha hiyo kuna wakati ilikuwa inaibua malalamiko kwa wanafunzi na kushukuru serikali kwa mikakati ya kunusuru hali hiyo.

"Chuo kinapata maji kutoka DUWASA na mwaka jana tulifanya utafiti mdogo ikaonekana watumiaji ni 39,000 na uwezo wa DUWASA ulikuwa kutupatia lita milioni 1.1 kwa siku wakati mahitaji halisi kwa muhimu wa utafiti huo mdogo ni lita milioni 2.29," alisema.

Prof. Kusiluka alisema kutokana na maji kutotosheleza, wamekuwa wakipata kutoka DUWASA kwa mgawo kwa wastani wa siku tatu kwa wiki na eneo la Ndaki ya Elimu ndilo linalokabiliwa na shida kubwa ya maji kutokana na wingi wa wanafunzi.

"Tumekuwa na juhudi za kutafuta maji na tuliandika barua sasa serikali ianze kuifikiria UDOM kwa namna tofauti kwenye suala la maji na jukumu likabidhiwa kwa RUWASA ambao walichimba visima vitano na kati ya hivyo, vinne vilionekana kuwa na maji kwa kiwango kidogo cha lita 40,000 na kuelekezwa Ndaki ya Elimu,"alisema.

Makamu Mkuu huyo alisema upungufu wa maji umekuwa ukisababisha baadhi ya wanafunzi kushindwa kusoma masomo ya maabara ambayo lazima kuwepo na maji na tishio la magonjwa ya mlipuko.

Alisema mpango mkakati wa chuo ni kutaka kuwa cha kimataifa na Rais Samia Suluhu Hassan ameshaidhinisha muundo wa uongozi wa vyuo vikuu vya umma na kila chuo kimeagizwa kuanzisha kitengo kinachoshughulikia masuala ya kimataifa.

## Wizara yaagiza kampuni za minara kupewa mikataba

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

WIZARA ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imeziagiza kampuni zote za mawasiliano nchini kutoa mikataba kwa wananchi wanaotoa maeneo yao kwa ajili ya kujenga minara.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Mhandisi Kundo Mathew, aliagiza hayo jana alipotembelea na kukagua mradi wa ujenzi wa mnara wa kampuni ya simu ya Airtel katika kata ya Sasilo, Manyoni mkoani Singida..

Alisema mikataba hiyo kabla ya kutiwa saini iwe inapelekwa mbele ya wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa katika maeneo husika ili kuwashauri wananchi vizuri juu ya ubora wa mikataba hiyo.

"Wananchi wa Sasilo hamna budi kuishukuru serikali kwa kuhakikisha mnapata huduma hii ya mawasiliano huku vijijini. Lakini pia kipekee kumshukuru mbunge wenu,. Dk. Pius Chaya, kwa kuwasemea kwani haikua rahisi kupata mradi huu wa Mnara ila kwakua alikua analisemea kila siku kwa uzito mkubwa," alisema.

Kundo alisema mnara huo utasaidia kata ya Sasilo na vijiji vyake na kwamba serikali itaendelea kuhakikisha kata na vijiji vingine ambavyo vina changamoto ya mtandao vinapata mtandao.

Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Thomas Apson, ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, alitoa shukrani kwa kukagua mradi huo na kujiridhisha kazi nzuri iliyofanyika na kuishukuru serikali na Airtel kujenga mnara huo ambao utawasaidia wananchi wilayani Manyoni.



Mbunge wa Isimani, William Lukuvi (kulia), akijadiliana jambo na Mbunge wa Morogoro Kusini, Innocent Kalogeris (kushoto) pamoja na Mbunge wa Mpanda Vijijini, Selemani Kakoso walipokutana Bungeni, jijini Dodoma jana, wanakohudhuria vikao vya kamati za Bunge. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Nchemba aagiza taasisi kusimamia haki

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAZIRI wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, ameigiza Taasisi ya Usuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi (TOST) kusimamia haki katika kufanya kazi zake ili kukuza uchumi na kuongeza pato ya nchini.

Aidha, amewataka wataalamu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA ) na taasisi hiyo kufanya marekebisho kwenye sheria ambazo zinaleta mkanganyiko katika ukusanyaji wa mapato.

Dk Nchemba alitoa maagizo hayo juzi wakati wa uzinduzi wa taasisi hiyo uliofanyika jijini hapa huku akiiagiza TOST kusimamia masuala ya sheria za kikodi ili kuinua uchumi wa nchi na kuongeza pato la taifa .

"Kwa sasa kuna shida ikitokea kesi kati ya serikali na mfanyabiashara na wakati mwingine inachukua muda mrefu ikitokea serikali ikashinda kutokana na mzigo kukaa muda mrefu unaweza kuharibika tukawa wote tumekosa kwa hiyo mkaliangalie hilo," alisema.

Kadhalika alisema taasisi hizo mbili zinapaswa kufanya kazi kwa ushirikiano mkubwa ili kuhakikisha wanafikia malengo ambayo serikali imejiwekea katika kuhakikisha uchumi wa nchi unakua.

Waziri aliziagiza taasisi hizo kufanya mchezo na watu ambao wanakwepa kulioa kodi,kwa sababu hakuna taifa linaloendelea bila ya kuwa na ulipaji kodi mzuri.

Aliongeza kuwa kutokana na kodi hizo serikali inaweza kuhudumia jamii kwa kujenga badabara ,kuongeza huduma za maji pamoja na kusambaza umeme maeneo ya vitongoji na vijiji.

Aidha, aliwataka wafanyabiashara kutoa risiti na upande wa wananchi kudai risiti kwa sababu kutokufanya hivyo ni kuikosesha nchi mapato .

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alisema uwapo wa tasisi hiyo itasaidia kupunguza malalamiko yaliyokuwa yanatolewa na wananchi kwenye mikutano mbalimbali.

**Dk Nchemba alitoa maagizo hayo juzi wakati wa uzinduzi wa taasisi hiyo uliofanyika jijini hapa**

Senyamule alisema wamekuwa wakipokea fedha nyingi za miradi ambayo inatekelezwa katika maeneo tofauti nchini .

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya kudumu ya Bajeti, Daniel Silo, alishauri taasisi hiyo kuhakikisha inatoa elimu kuhusu kazi inazofanya na zaidi kutumia mifumo ya kieletroniki katika kupokea malalmiko ya wananchi.



HABARI MBEYA

# Mganga mkuu atumbuliwa kisa ujenzi wa choo

**Na Nebart Msokwa,**
BUSOKELO

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, amegeuka mbogo na kumtumbua Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe, Dk. Meshack Mwasongela, kwa kushindwa kutekeleza amri ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa.

Mwanzoni mwa Desemba, mwaka jana, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya iliagiza choo kijengwe katika zahanati ya Ntapisya iliyoko Kata ya Lupata Katika Halmashauri ya Busokelo ili zahanati hiyo ianze kutoa huduma.

Kamati hiyo iliagiza zahanati hiyo ianze kufanya kazi Januari 15, mwaka huu, kwa kupelekwa dawa, vifaa tiba na watumishi ili wananchi wa eneo hilo waache kutembea umbali mrefu kwenda kutafuta huduma za afya.

Juzi Homera alirudi Busokelo kuangalia kama maagizo hayo yametekelezwa na kukuta hakuna chochote kilichofanyika.

"Tuliagiza ujenzi wa choo katika zahanati ile (Ntapisya) ukamilike haraka na kufikia Januari 15 zahanati ile iwe imeanza kuwahudumia wananchi, mpaka sasa hakuna kilichofanyika. Sasa naagiza RAS (Katibu Tawala Mkoa) amwondoe hapa huyu DMO na badala yake ateuliwe mwingine afanye kazi hii," alisema.

Homera alisema hawezi kurudi katika Zahanati ile na kuzungumza na wananchi ambao aliwaahidi kuwa itaanza kazi ndani ya muda aliowaeleza, ahadi ambayo haikutekelezwa kama alivyoitoa.

Pamoja na kutokukamilika kwa ujenzi wa choo hicho, aliagiza zahanati hiyo ifunguliwe huku akiagiza uongozi wa halmashauri kuweka mikakati ya kujenga miundombinu hiyo.

Dk. Mwasongela alisema wameshafanya maandalizi yote ya kuifungua zahanati hiyo ikiwamo kuandaa vifaa tiba na watumishi na kwamba walikuwa wanasubiri wakamilishe ujenzi wa choo ili waifungue.

Alisema wanakusudia kuifungua zahanati hiyo hivi karibuni baada ya kukamilisha ujenzi wa miundombinu hiyo muhimu na kwamba vifaa vya ujenzi tayari wameshanunua.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Elizabeth Mnyema, alisema amekuwa akifuatilia mara kwa mara utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa ikiwamo kukamilisha ujenzi wa zahanati hiyo.

Alisema kilichosababisha ichelewe kufunguliwa ni kutokukamilika kwa ujenzi wa choo na kwamba kwa sasa wanakusudia kuifungua hivi karibuni.

"Kwa sasa tumeshafanya utaratibu wa kuwapanga wafanyakazi wa kwenda kufanyakazi kwenye ile zahanati, walikuwa wanaendelea kuleta mchanga na matofali kwa ajili ya kukamilisha choo," alisema Dk. Mnyema.




Meya wa Jiji la Mbeya, Shekhe DorMohamed Issa akizungumza na wananchi wa kata ya Nonde, jijini humo juzi, wakati akihamasisha ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya maendeleo ikiwemo shule. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Barabara mpya za lami kufungua uchumi wa Nyanda za Juu Kusini

**Na Elizabeth John,** LUDEWA

SERIKALI imeweka mikakati madhubuti ya ujenzi wa barabara katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ili kuruhusu shughuli za kiuchumi zilizofungwa miaka mingi kufunguka ukiwamo mradi pacha wa Liganga na Mchuchuma.

Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, alisema hayo juzi alipotembelea barabara ya Itoni hadi Lusitu yenye urefu wa kilometa 50 inayojengwa kwa kiwango cha zege kwa thamani ya Sh. bilioni 100 kuunganisha Njombe na Ludewa.

Bashungwa alisema mradi wa Liganga na Mchuchuma ni zaidi ya miaka 40 umekuwa ukizungumzwa bila ya kutekelezeka.

"Ili kuwavutia wawekezaji ni lazima tupeleke miundombinu mpaka kwenye eneo la mradi jambo ambalo miaka mingi zaidi ya 40 limeshindikana. Lakini mfupa huu Mheshimiwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan anakwenda kuuvunja," alisema.

Bashungwa alisema katika mikakati ya serikali katika mpango wa kuunganisha mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, kuna mpango wa kujengwa upya barabara Songea- Njombe hadi Makambako.

"Tuko mbioni kumpata mkandarasi ili kufumua barabara ya Songea kuja Njombe mjini mpaka Makambako inakuja kujengwa upya kwa mabilioni na mabilioni," alisema Bashungwa.

Pia alibainisha kwamba serikali itajenga barabara kutoka Kibena hadi Lupembe (kilometa 42) kwa thamani ya Sh. bilioni 75 ili kuunganisha na Mkoa wa Njombe Morogoro.

Bashungwa alisema serikali pia ameridhia kutoa Sh. bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Mlangali - Lupila hadi Ikonda.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, alisema wilaya ya Ludewa ndiko kuliko na mradi wa Liganga na Mchuchuma.

"Kukamilika kwa barabara hii kutafungua mkoa wa Njombe lakini Mheshimiwa Waziri utaona kwenye dira mpya ya maendeleo moja ya uchumi mpya unaozunguzwa ni uchumi wa madini yaliyoko Mchuchuma na Liganga," alisema Mtaka.

Awali, Kaimu Mkurugenzi wa Miradi wa Wakala wa Barabara (TANROAD), Japhason Nnko, alisema barabara ya Itoni- Lusitu hadi Manda yenye urefu wa kilomita 211, hususani kipande cha Itoni - Lusitu (km 50) imesanifiwa kwa upana mita 11.

"Mita saba kamili ni kwa ajili ya magari na mita nne kwa maana ya mita mbili kila upande ni kwa ajili ya watembea kwa miguu," alisema Nnko.

# RC aonywa wananchi kuendekeza migogoro

**Na Elizabeth John,**
WANG'ING'OMBE

WANANCHI wilayani Wang'ing'ombe katika Mkoa wa Njombe, wametakiwa kuheshimu mpango wa matumizi bora ya ardhi ambao wamekubaliana ili kuepuka migogoro ya ardhi.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, alisema hayo juzi wakati akisikiliza kero za wananchi wa kitongoji cha Halali, kijiji cha Mayale wilayani hapa.

Mtaka alisema wananchi wa Wang'ing'ombe kwa kuwa hali yao inaruhusu joto, wasipoheshimu mpango wa matumizi bora ya ardhi waliyokubaliana, migogoro ya ng'ombe iliyopo Mbarali itahamia katika wilaya hiyo.

Alisema wananchi wanakubaliana kutenga eneo kwa ajili ya ufugaji na kilimo lakini wanatokea watu na kukiuka makubaliano hayo.

"Mnakubaliana kwamba eneo hili ni la wafugaji, eneo hili ni la wakulima , eneo hili ni la taasisi , hili la makazi na hili la makaburi. Lakini wanatokea watu wanakwenda kwenye eneo ambalo mmekubaliana kwamba mtafuga, wanaenda kufyeka pori na kulima," alisema.

Mtaka alisema maeneo yote ambayo vijiji vimepanga kwa ajili ya matumizi bora ya ardhi na wananchi wakaridhia, yanatakiwa kuheshimiwa na watakaokiuka wachukuliwe hatua.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, Peter Nyanja, alisema moja ya mikakati aliyo nayo ni kukuza mji wa Wang'ing'ombe na wilaya yake kwa ujumla.

Alisema halmashauri kwa kushirikiana na vijiji, itatoa maeneo kwa wawekezaji kwa bei rahisi ili kuwavutia kufanya shughuli kwenye halmashauri na miji kukua.

"Lakini kingine katika kukuza mji wetu wa Wang'ing'ombe tunalo zao la viazi na sasa hivi teknolojia imekua tunaenda kuvioka na kuvipaki kwa hiyo watu watakwenda kuvitumia kwenye familia na kwenye masoko," alisema Nyanja.

Diwani wa Wang'ing'ombe, Geofrey Nyagawa, alisema kata inakabiliwa na mgogoro wa ardhi hasa kwa wakulima.

"Mgogoro mkubwa uliopo hapa niliomba watu wa ardhi waje kutatua migogoro ya ardhi iliyopo hasa ya wakulima," alisema Nyagawa.

Mmoja wa wananchi wa kitongoji cha Halali, Oscar Mbafu, alisema licha ya kuwapo kwa mpango wa matumizi bora ya ardhi katika kijiji hicho lakini eneo kwa ajili ya wafugaji limevamiwa na shughuli za kilimo zinafanyika.



# Mjumbe NEC CCM akemea makundi

**Na Mwandishi Wetu**

MJUMBE wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (NEC), Tauhida Galos Nyimbo, amewataka watendaji na kamati tekelezaji wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Mkoa wa Kichama wa Magharibi Unguja, kuwaunganisha viongozi wao ili kuleta maendeleo na si kuwagawa makundi.

Akizungumza jana Mwera visiwani hapa wajumbe hao katika wilaya za Dimani na Mfenesini, alisema kuna baadhi ya watendaji wanawaandaa watu wao kugombea katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwakani jambo ambalo linasababisha kuwagawa makundi viongozi.

Nyimbo ambaye pia ni Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Magharibi, alisema wakati wa kampeni haujafika, hivyo wanapaswa kushirikiana na viongozi waliopo madarakani kutatua matatizo ya wananchi.

'Wanawake wenzangu, kuna matatizo tele yanayowakabili wanawake wenzetu. Tushuke chini kuwasaidia kwa mustakabali wao na taifa kwa ujumla," alisema.

Pia aliwataka viongozi hao kutatua matatizo mbalimbali yanayowakabili wananchi ili kuunga mkono utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025.

Alisema Wabunge, Wawakilishi na Madiwani wa UWT katika mkoa huo ni kitu kimoja lakini baadhi ya watendaji wanawatia chokochoko viongozi hao kwa maslahi yao binafsi.

''Jamani acheni chokochoko si nzuri. Huu ni wakati wa kukijenga chama chetu ili tuzidi kukipatia ushindi ifikapo mwaka 2025,'' alisisitiza.

Wajumbe wa Kamati Tekelezaji katika wilaya za Dimani na Mfenesini kichama waliahidi kuyafanyia kazi maelekezo waliyopewa sambamba na kupita nyumba kwa nyumba kuhamasisha wananchi kujiunga na umoja huo.

Aidha waliwataka viongozi kufanya ziara za mara kwa mara ili kubaini matatizo waliyo nayo wananchi na kuyatafutia ufumbuzi wa haraka kwa faida ya UWT na CCM kwa ujumla.

# Z'bar yavunja rekodi kuingiza watalii

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

ZANZIBAR imevunja rekodi ya watalii kwa kuingiza watalii 638,498 kwa mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 16.4 kulinganisha na mwaka 2022 walipokuwa 548,503.

Mkuu wa Divisheni ya Takwimu za Utoaji Huduma katika Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Bakari Khamis Kondo, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu takwimu za uingiaji wa wageni.

Alisema kati ya wageni hao walioingia mwaka jana, bara la Ulaya linaongoza kwa kuwa na wageni 392,907 waliotoka sawa na asilimia 71.6 ya wageni wote wakifuatiwa na Afrika watalii 72,814 sawa na asilimia 13.3.

Kondo alisema kwa upande wa Asia walikuwa 37,080 sawa na asilimia 6.8 na Oceania walikuwa 2,745 sawa na asilimia 0.5 ya wageni wote.

Pia alisema nchi tano zilizoongoza kwa kuwa na wageni wengi ni Ufaransa wageni 68,487 (asilimia 12.5) ikifuatiwa na Poland wageni 44,462 (asilimia 8.1) na Ujerumani 43,634 sawa na asilimia nane.

"Italia ni ya nne kwa kuingiza wageni 36,928 sawa na asilimia 6.7 na ya tano ni Uingereza iliyoingiza wageni 30,562 sawa na asilimia 5.6," alisema.

Pia alisema wageni 570,394 sawa na asilimia 89.3 ya wageni wote walioingia Zanzibar walipitia viwanja vya ndege na wengine 68,104 sawa na asilimia 10.7 waliingia kupitia bandarini.

Alisema wageni 319,979 sawa na asilimia 50.1 walikuwa na jinsia ya kiume na wageni 318,519 sawa na asilimia 49.9 ni wa jinsi ya kike.

Kwa mujibu wa Kondo, madhumuni ya safari za wageni hao, asilimia 97.8 yalikuwa kwa ajili ya mapumziko, asilimia 0.4 kutembelea ndugu na marafiki na asilimia 1.7 kwa sababu zingine na walikaa Zanzibar kwa wastani wa siku moja hadi 10.

Serikali ya Zanzibar ilijiwekea lengo la wageni 450,000 kwa mwaka 2023 lakini imevuka lengo hilo na kwa mwaka huu wa 2024 lengo ni kupokea wageni 650,000 na inakusudia kuongeza bidhaa za utalii ili kuvutia watalii wengi zaidi.



Mstahiki Meya wa Jiji la Zanzibar, Mahmoud Mohammed Musa (wapili kushoto), akikata utepe kuzindua kituo kipya cha huduma kwa wateja cha kampuni ya Tigo Zantel Zanzibar jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa Huduma kwa wateja wa kampuni hiyo, Mwangaza Matotola. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Wataka mikoa kuongeza ulinzi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAMATI ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi imewataka watendaji wa mikoa wakiwamo wakuu wa mikoa na wilaya kuongeza ulinzi katika maeneo yao.

Viongozi hao wamesema lengo la kufanya hivyo ni kudhibiti matukio ya uhalifu ambayo yanaweza kuzorotesha maendeleo ya sekta mbalimbali ikiwamo utalii.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Machano Othman Said, wakati wa majumuisho ya ziara yao mbele ya uongozi wa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Alisema viongozi wa mikoa na maeneo yao wanatakiwa kujipanga kuona nchi inakuwa salama dhidi ya matukio yote ya uhalifu yanayotishia amani na utulivu.

Machano alisema katika nyakati tofauti kumeripotiwa kujitokeza matukio ya uhalifu vikiwamo vikundi vinavyoranda randa mitaani na kuwapiga watu pamoja na kuwanyang'anya mali zao.

Alisema matukio ya vijana wa kihuni kwa sasa hayakubaliki na huu ni wakati mwafaka kwa watendaji wa mikoa kuhakikisha yanadhibitiwa.

"Hivi karibuni tumesikia na wananchi kutoa malalamiko dhidi ya baadhi ya vijana kupita usiku katika nyumba zao na kuwalazimisha kutoka nje na kuwapiga pamoja na kuwanyang'anya mali zao. Tunajiuliza viongozi wetu na vikosi vyetu viko wapi?" alihoji.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mariyam Thani Juma, alisema Zanzibar imefanikiwa kutangaza utalii huku idadi kubwa ya wageni wakiwasili, hivyo ulinzi unatakiwa kuimarishwa.

"Kila siku tunashuhudia tunapokea wageni wakiwamo watalii katika maeneo mbalimbali ikiwemo Mji Mkongwe, hivyo tunatakiwa tujipange kiulinzi," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Rashid Hadid Rashid, alisema wamejipanga kuhakikisha ukanda wa mkoa wa kaskazini likiwamo eneo la Nungwi, unakuwa salama na matukio ya uhalifu.

Alisema mkoa kwa kushirikiana na kikosi cha Polisi Utalii, wanafanya kazi nzuri ya doria katika kudhibiti matukio ya uhalifu na kwa kufanya hivyo, katika mwaka 2023 hakuna uhalifu ulioripotiwa.

"Mkoa wa Kaskazini Unguja wenye hoteli nyingi za kitalii, tumefanikiwa kudhibiti uhalifu kwa kufanya kazi na kikosi cha Polisi Utalii kiasi kwamba katika mwaka uliopita hakuna matukio ya uhalifu ya kupigwa kwa watalii au kuporwa mali zao yaliyoripotiwa," alisema.

Awali, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum SMZ, Masoud Ali Mohamed, alisema serikali imejipanga kwa kuvitumia vikosi vyake na Jeshi la Polisi katika kuimarisha doria.

Alisema vikosi vya Idara maalum SMZ vimeanza kufanya doria zaidi katika maeneo ambayo yanatajwa kuwapo kwa vikundi vinavyojishughulisha na vitendo vya kihuni zaidi nyakati za usiku.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya MWANGA
Kituo cha MWANGA
Mkoa KILIMANJARO
Usimamizi wa mirathi Na 01/2024
KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA
MAREHEMU OMARY DANIEL KIVARIA MVUNGI WA MWANGA
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI
YALIYOLETWA
NA MOHAMED OMARY DANIEL

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 05 Mwezi 02 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa

Imetolewa leo tarehe 05 Mwezi 01 Mwaka 2024

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
MWANGA

## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**D4N COMPANY LIMITED** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI ZA MAGARI. GARI AINA MITSUBISH FUSO YENYE NAMBA YA USAJILI T 474 DFY. TAARIFA YA POLISI KAH/40/2024. GARI AINA YA VOLKS WAGEN YENYE NAMBA ZA USAJILI T 418 DGE. KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI **KAH/TR /RB/39/2024.**

## TANGAZO KUPOTELEWA NYARAKA YA UMILIKI KIWANJA

**Bundala Kali Kali** ambaye ni Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu Bundala Ndenge. Anatangaza kupotelewa na Nyaraka ya Umiliki wa Kiwanja namba 73 Kitalu "T" kilichopo Majengo Manispaa ya Shinyanga. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Bundala kwa simu namba 0767-593474.

**Taarifa ya Polisi:PHQ/SHI/SHI/247/2024.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**MASALU NAPHTALI MASANJA** ANATANGAZA KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA YENYE NO TAE 393519 ILIYOTOLEWA NA IDARA YA UHAMIAJI DAR-ES-SALAAM .
KWA ATAKAYEIONA ANAOMBWA ATOE TAARIFA KATIKA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI . **PHQ/ARU/MER/1669/2024**

## KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO (LETTER OF OFFER)

**HASANI KAMBI KASEGE** anatangaza kupotelewa na offer ya Kiwanja namba 78 Kitalu "D" kilichopo Njombe Mjini. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya polisi **PHQ/NJO/NJO/54/2024.**

JAMHURI YA MUUNGANOI WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika Mahakama ya mwanzo ya wilaya ya DODOMA MJINI
Kituo cha JUMUISHI
Mkoa DODOMA
Usimamizi wa Mirathi No. 04/2024
KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA
MAREHEMU NYOKA SELEMANI SHIJA wa DODOMA
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMSMIZI
YALIYOLETWA
NA SAUDA SAIDI SWALEHE

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote /maslahi yoyote na Mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 07 mwezi 2 mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa Msimamizi wa Mirathi hiyo.

**ZINGATIA;**

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuleta Mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo tarehe 24 mwezi 1 mwaka 2024

## KUPOTEA KWA KADI ZA GARI

**OMAR IDD KAKIVA** anatangaza kupotea kwa kadi za gari aina ya TOYOTA LANDCRUISER zenye jina la umiliki DONAK SAFARIS LIMITED zenye namba za usajili T 357 BDF na T 787 CLY, CHASSIS NAMBA : JTERB71JX00053527 na JTERB71J500049210 na ENGINE NAMBA: 1HZ0624421 na 1HZ0600253. Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/ARU/AR/1872/2024**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika Mahakama ya Mwanzo KAWE Wilaya ya KINONDONI
Kituo cha KAWE Mkoa DAR ES SALAAM
Shauri la Madai/Ndoa Na. 07, 2024
Jina la Mdai NICKSON JACKSON KAWICHE
Jina la Wadaiwa: TUMAINI LEMA NA AMANI URASSA

**KUITWA SHAURINI WADAIWA**

**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za Taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: TUMAINI LEMA NA AMANI URASSA – GOBA DAR ES SALAAM**

**Kwa kuwa Mdai/Wadaiwa ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba**

**KUJA KUJIBU MADAI YA PESA SH. 2,380,000/ ILIYOFUNGULIWA HAPA MAHAKAMANI**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 05 Mwezi 02 Mwaka 2024 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

Angalizo: Kama hautahudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 22 Mwezi 01 Mwaka 2024.

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

***Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701***

**KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTE KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.**
**TUPIGIE: +255 - 0677020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Waasi wa M23 waunda serikali yao Kivu Kaskazini

**GOMA,** DRC

WASIWASI umetanda nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) baada ya waasi wa M23 kuunda serikali yao itakayoendeshwa katika maeneo yaliyo chini ya udhibiti wake.

Katika taarifa ya kundi hilo, kiongozi wa kisiasa wa M23 Bertrand Bisimwa, alisema kundi hilo limeteua viongozi ambao watatawala eneo la Rutshuru liloko katika jimbo la Kivu Kaskazini.

Aliongeza kuwa viongozi wengine walioteuliwa ni wa miji ya Kiwanja, Rubare na Bunagana.

Waasi hao wanadhibiti sehemu kubwa ya Rutshuru na Masisi, ambazo ni wilaya mbili kati ya tano zinazounda jimbo la Kivu Kaskazini.

Maeneo hayo yako kilomita 35 magharibi mwa mji mkuu wa Goma.

Katika siku za hivi karibuni, jeshi la Congo limeanzisha mashambulizi makali a ndege zisizo na rubani katika maeneo yanayodhibitiwa na M23.

Jumatano msemaji wa kundi hilo alisema wapiganaji wake waliiangusha ndege moja kati ya tatu zilizokuwa zikitumiwa na jeshi la DRC.

Hata hivyo, BBC haijathibitisha madai hayo na jeshi la serikali halijasema chochote.

Mitandao ya kijamii chini humo imekuwa ikijibu taarifa hiyo ya M23 kuteua utawala wake katika maoni tofauti.

Baadhi wanaona hatua hiyo ni mwanzo wa waasi hao kuunda jimbo jipya na kulitenga nan chi yao. **BBC**



Kiongozi wa M23, Betrand Bisimwa

# Israel yazidisha mashambulizi baada wanajeshi wake 21 kuuawa na Hamas

**TEL AVIV,** Israel

JESHI la Israel limeendelea kufanya mashambulizi makali katika mji wa Khan Younis uliopo Ukanda wa Gaza baada ya juzi askari wake 32 kuuawa na wanamgambo wa Kipalestina.

Katika tukio hilo, wanamgambo wa Kipalestina walifanya shambulizi la kushtukiza dhidi ya vikosi vya Israel katika Ukanda wa Gaza na kusababisha vifo hivyo ambavyo viliishtua serikali ya Israel.

Saa chache baada jeshi la Israel kutangaza kupoteza idadi kubwa ya askari walioko katika mstari wa mbele, vikosi vya jeshi la ardhini waliuzingira mji wa Khan Younis ambao ni wa pili kwa ukubwa Ukanda wa Gaza.

Jana katika mji huo kulisikika milipuko ya mabomu na moshi mzito ukitanda angani, huku maelfu ya Wapalestina wakikimbilia upande wa kusini.

Mashuhuda walisema kwamba vifaru vya Israel na vikosi askari wameingia eneo la karibu la pwani la Muwasi ambalo awali lilikuwa limetangazwa na jeshi kuwa sehemu salama kwa Wapalestina.

Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu alioomboleza vifo vya askari hao kwa kusisitiza kwamba mapigano yataendelea hadi utakapopatikana ushindi kamili.

Katika tukio hilo wapiganaji wa Hamas walifyatua roketi ambayo ililipua mabomu ambayo yangetumika na Israel kushambulia majengo.

Netanyahu ameapa kuliangamiza kundi la Hamas na kuwaokoa mateka zaidi ya 100 ambao bado wanashikiliwa na wanamgambo.

"Tumo katikati ya vita ambayo bila shaka ni halali, tunapata mafanikio kama vile kuizingira Khan Yunis na pia tumepata hasara kubwa. Tunainamisha vichwa vyetu kuwakumbuka waliokufa, na bado hatuachi kujitahidi kufikia lengo letu la kupata ushindi kamili. Pamoja tutapigana na kwa mapenzi ya Mungu, sote tutashinda", alisema Netanyahu.

Hata hivyo raia wa Israel wanazidi kuhoji ikiwa nchi hiyo itaweza kufikia malengo hayo ya vita.

Wakati mapigano yakizidi kushika kasi, Shirika la misaada ya kiutu la Umoja wa Mataida (OCHA), limeripoti kwamba vikosi vya Israel vilimetoa maagizo mapya ya watu kuhama sehemu ya makazi yao katika mji wa Khan Yunis.

Mji huo unakadriwa kuwa na watu nusu milioni na wengine walikimbia mapigano.

Maagizo hayo yametolewa wakati shirika jingine la Mpango wa Chakula duniani, lilionya kuwa raia wa Gaza wanakabiliwa janga la njaa kutokana na kukosa chakula.

Shirika la habari la Palestina (Wafa), limeripoti kwamba ofisi ya rais wa Mamlaka ya Palestina Mahmud Abbas imeshutumu masharti ya kuhama na kuweleza ni ya hatari watu kuelekea kusini.

Ilionya kwamba nchi ya Israel inakusudia kuwaondoa Wapalestina kutoka ardhi yao na hivyo kusababisha matokeo yasiyotarajiwa.

Vita hivyo vilianza baada ya shambulizi la kushutukiza lililofanywa na Hamas Oktoba 7 na kuwaua watu zaidi ya 1000 wa Israel.

Taarifa kutika vyanzo tofauti vinasema kundi la Hamas limeonyesha nia ya kufanya mazungumzo na Israel ya kuwaachia baadhi ya mateka.

Jarida la Wall Street liliripoti juzi likiwanukuu maafisa wa Misri kuwa Hamas iliwaeleza wapatanishi kuwa wanaweza kufanya mazungumzo ya kuwaachia mateka wa kike na watoto kwa sharti la kusitisha mapigano.

Hadi sasa Hamas imeshawaachia mateka 105 wakati wa usitishaji mapigano ya kipindi cha wiki moja mwishoni mwa Novemba mwaka jana. **DW**



Raia wanaokimbia mapigano katika mji wa Khan Younes, wakijiandaa kuelekea eneo la Rafah jana. **PICHA: AP**

# Kagame aapa kulinda nchi hata kwa kupigana

**KIGALI, Rwanda**

WAKATI kuna mvutano kati ya nchi ya Rwanda na jirani zake Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Burundi, Rais Paul Kagame, ameapa kulinda nchi yake dhidi ya uchokozi kutoka mataifa ya nje.

Akiwahutubia wajumbe katika mkutano wa majadiliano ya kitaifa mjini Kigali jana, Kagame alisema hawatahitaji ruhusa ya mtu yoyote linahusu kuitetea nchi yao.

"Linapokuja suala la kuitetea nchi hii ambayo imeteseka kwa muda mrefu na hakuna aliyekuja kusaidia, hatuhitaji ruhusa kutoka kwa mtu yeyote kufanya kile tunachotakiwa kufanya ili kujilinda," alisema Kagame katika hotuba iliyorushwa na televisheni ya taifa ya nchi hiyo juzi.

Rais Kagame kwa mara nyingine alikanusha madai yanayotolewa na DRC kuwa nchi yake inawaunga mkono waasi katika maeneo ya mashariki mwa Congo.

Akizungumzia mauaji ya kimbari ya mwaka 1994 yaliyofanywa dhidi ya Watusi, kiongozi huyo alisema kuwa kama kuna atakayetufanya na kuwarudisha nyuma katika nyakati hizo, basi hawana cha kupoteza na watapopigana kwa nguvu.

Rwanda imeingia katika mzozo wa kidiplomasia na Burundi, ambayo ilifunga mpaka wake Januaria 11 baada ya kuihusishwa na shambulio la kigaidi lililofanywa na waasi wa RED-Tabara mwezi Disemba.

Hata hivyo, Burundi ilikanusha jana kuhusu madai ya Rwanda yanayomtuhumu Rais Evariste Ndayishimiye kuwa alitoa wito wa kuondolewa madarakani Rais Kagame wakati wa akizungumza na vijana aliopofanya ziara nchini DRC Januari 21. **BBC**



# KIPENGA MICHUANO KOMBE LA FA ZANZIBAR KUMEKUCHA

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

HATUA ya awali ya mashindano ya kuwania ubingwa wa Kombe la ZFF (FA CUP) msimu huu imepangwa kufanyika kuanzia leo na itachezwa kwa mfumo wa mtoano, imeelezwa.

Michuano hiyo inachezwa kwa kanda mbili, ambapo mshindi wa Kanda ya Unguja atacheza dhidi ya mshindi wa Kanda ya Pemba ili kupata timu itakayoiwakilisha Zanzibar katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu wa Kamati ya Mashindano Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Ali Bakari, alisema taratibu zote kuelekea mashindano hayo kwa Unguja na Pemba zimekamilika.

**Bakari alisema michuano katika hatua ya awali inashirikisha timu 40 kutoka kwenye Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja pamoja na timu kutoka mikoa mitatu ya Unguja ambayo ni Mkoa wa Mjini Magharibi, Mkoa wa Kaskazini na Kusini Unguja.**

Alisema kwa mujibu wa ratiba, hatua hii ya awali michezo yake itamalizika ifikapo Januari 29, mwaka huu ili kupata timu ambazo zitaingia katika mzunguko wa pili wa michezo wa michuano hiyo itafanyika kwenye viwanja mbalimbali kwenye mikoa Unguja kutokana na ratiba ilivyopangwa.

"Tayari timu zote zimeshapewa ratiba ya kuanza rasmi mbio za michuano hii ya FA kwa msimu huu, kikubwa tumewasisitiza kuheshimu na kufata kanuni ya mashindano haya ili kuhakikisha taratibu zote za mchezo zinafuatwa kama zilivyo"alisema Bakari.

Aliongeza timu za Ligi Kuu Zanzibar zitaanza kushiriki katika mzunguko wa pili wa michuano kama kanuni ya mashindano kwa msimu huu wa 2023-2024 zinavyoeleza.

Kiongozi huyo amewaomba wadau wa soka mbalimbali kujitokeza kudhamini michuano hiyo kuanzia ngazi ya awali ili kuleta ladha na hamasa ya mashindano kama ilivyo kwa Ligi Kuu Zanzibar na mashindano mengine ambayo yamepata udhamini.

Alitaja mechi zitakazochezwa leo ni kati ya Shangani dhidi ya Jang'ombe Boys mchezo utakaofanyika kwenye Uwanja wa Mau A wakati Bambuu itawakaribisha Mbweni Academy na Black Mamba wataivaa Desi FC huku Black Sailor ikiwaalika Kilimani Fighter kwenye Uwanja wa Kinyasini, Kinyasini.

# Mashujaa yasajili saba wapya

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Mashujaa inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara imeweka rekodi ya kusajili idadi kubwa ya wachezaji kipindi cha dirisha dogo la usajili ikiamini itawasaidia kujiondoa na hatari ya kushuka daraja, imefahamika.

Mashujaa yenye maskani yake mkoani Kigoma imesajili nyota wapya saba na katika kujiwinda na hatua ya lala salama imeweka kambi jijini Dar es Salaam, tayari kumalizika msimu baada ya mechi za Ligi Kuu kurejea tena kutokana na kupisha fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON).

Wachezaji wapya waliosajiliwa na timu hiyo ni pamoja na Nyeyezi Juma kutoka Inter Star ya Burundi, Emmanuel Mtumbuka (Stand United), Mpoki Mwakinyuke, Samson Madeleke, Omari Abdallah ( Prisons), Reliants Lusajo (Namungo) na golikipa, Patrick Muntari.

Kocha Mkuu wa Mashujaa, Mohammed Abdallah 'Bares', amesema usajili wote umefanyika kwa manufaa ya klabu, hasa baada ya kuangalia mapungufu yaliyojitokeza katika mechi zilizopita.

"Ilikuwa lazima tufanye usajili mkubwa kwa sababu hatukuwa na watu wengi wenye uzoefu wa ligi na kadri mechi zilivyozidi kuendelea udhaifu huu ulionekana zaidi," alisema kocha huyo.

Mashujaa inajiandaa kuwakabili Geita Gold ifikapo Februari 17, mwaka huu kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika.




Mkurugenzi wa Kampuni ya Tigo Kanda ya Pwani, Aidan Komba (kushoto) akimkabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni tano, mshindi wa Promosheni ya Magift Dabodabo, Hamisa Haule . **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mtibwa, Ihefu SC kujipima Feb. 13

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Mtibwa Sugar inatarajiwa kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya Ihefu SC itakayochezwa Februari 13, mwaka huu kwenye Uwanja wa Manungu Complex, Morogoro ili kujiandaa na hatua ya lala salama ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na Nipashe jana, Msemaji wa Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru, alisema wanaendelea kufanya mazungumzo na timu nyingine ambazo wanahitaji kujipima kabla ya kurejea kwa Ligi Kuu Bara.

"Mwishoni mwa wiki hii tunatarajia kucheza mchezo wa kirafiki na timu ambayo tutacheza nayo tutawajulisha mazungumzo yatakapokamilika, lakini tayari tumeshakubaliana kujipima na Ihefu," alisema Kifaru.

Aliongeza wamefanya usajili mzuri ambao utawaongeza nguvu kutokana na aina ya wachezaji waliojiunga na timu hiyo ambayo haikuwa na msimu mzuri katika mzunguko wa kwanza.

Aliongeza bado uongozi na wachezaji wa timu hiyo hawajakata tamaa na wamejipanga kuendelea kupambana ili kufikia malengo na pia wamewaomba mashabiki wai kuwaunga mkono.

# Ligi ya Kikapu Dar yapigwa kalenda

**Na Shufaa Lyimo**

LIGI ya mpira wa wavu Mkoa wa Dar es Salaam iliyopangwa kufanyika kuanzia Februari 10, mwaka huu imesogezwa mbele mpaka February 17, mwaka huu, imeelezwa.

Mwenyekiti wa Chama cha Wavu Mkoa wa Dar es Salaam (DAREVA), Fred Mshangama, aliliambia gazeti hili sababu ya kusogeza mbele ligi hiyo ni kupisha timu za taifa zinazotakiwa kusafiri kwenda nje ya nchi kupeperusha bendera ya Tanzania.

Mshangama alisema Timu ya Taifa ya mchezo huo inatarajia kuelekea Rwanda kushiriki mashindano maalum yatakayofanyika baadaye mwezi huu.

"Tumelazimika kupangua ratiba kwa sababu hii kubwa. Tunaamini baadhi ya timu zitawakosa wachezaji wao wengi muhimu, hivyo tumetoa nafasi kusubiri mpaka hapo watakaporejea," alisema Mshangama.

Aliongeza timu 25 za Wanaume na Wanawake zimethibitisha kushiriki ligi hiyo ambayo inatarajiwa kuwa na upinzani lakini wamekumbushwa kulipa ada ya ushiriki.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### CASEMIRO, BISSAKA KUUZWA

KLABU ya Al-Nassr inajipanga kwa dau la kutaka kumnunua kiungo wa kati wa Brazil, Casemiro mwenye umri wa miaka 31 na beki wa England, Aaron Wan-Bissaka (26), huku Manchester United ikipanga kuwauza baadhi ya nyota wake wanaolipwa fedha nyingi. ***(Mail)***

### WAMKATAA EMERSON

AL-Nassr tayari wamekataa ofa ya pauni milioni 20 kumnunua beki wa kulia wa Tottenham Hotspur na Brazil, Emerson Royal, mwenye umri wa miaka 25 na wanamtazama Aaron Wan-Bissaka kama mbadala wake. ***(Telegraph)***

### OSIMHEN KUONDOKA NAPOLI

VICTOR Osimhen amedokeza yuko tayari kuondoka Napoli msimu huu wa joto, huku Chelsea, Manchester United na Real Madrid zikihusishwa na mshambuliaji huyo wa Nigeria mwenye umri wa miaka 25, ambaye ana kipengele cha kuachiliwa cha zaidi ya pauni milioni 100 katika mkataba wake. ***(90min)***

### GREENWOOD ANUKIA BARCA

MSHAMBULIAJI wa Manchester United ambaye yuko kwa mkopo, Mason Greenwood, mwenye umri wa miaka 22 anakaribia kuhamia Barcelona majira ya joto baada ya kuichezea Getafe. ***(Sun)***

### REYNA KUTUA FOREST

KLABU ya Nottingham Forest iko kwenye mazungumzo na Borussia Dortmund kuhusu mkataba wa mkopo wa kiungo wa kati wa Marekani, Giovanni Reyna, mwenye umri wa miaka 21. ***(Athletic)***

### HODGSON MAMBO MAGUMU

KOCHA wa Crystal Palace, Roy Hodgson, mwenye umri wa miaka 76 ameonywa huenda akafutwa kazi ikiwa matokeo hayataboreka baada ya kufanya mazungumzo na Mwenyekiti, Steve Parish. ***(Guradian)***

### DENDONCKER SOKONI RASMI

KLABU ya Napoli imekubali mkataba wa mkopo na Aston Villa, ambao unajumuisha chaguo la kumnunua kwa kipengele cha thamani ya pauni milioni 7.7 kiungo wa kati wa Ubelgiji mwenye umri wa miaka 28, Leander Dendoncker. ***(Fabrizio Romano)***

### NUSA ATAJWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inafikiria kumnunua mshambuliaji wa Club Bruges, Antonio Nusa mwenye umri wa miaka 18. Nyota huyo wa Norway anaonekana kuchukua nafasi ya moja kwa moja ya mchezaji wa kimataifa wa Paraguay, Miguel Almiron (29), ambaye huenda akaondoka pale Tyneside na kujiunga na Al-Shabab ya Saudi Arabia. ***(Football Insider)***

### BENZEMA ATAKIWA CHELSEA

CHELSEA imeonyesha nia yao ya kutaka kumsajili mshambuliaji wa Ufaransa, Karim Benzema, mwenye umri wa miaka 36 kutoka klabu ya Al-Ittihad ya Saudi Arabia. ***(Guradian)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# GHANA YAONDOLEWA, YAMTIMUA HUGHTON

**ACCRA,** Ghana

## ● ● ● Ni baada ya kocha huyo kushindwa kuipeleka mbele katika...

TIMU ya Taifa ya Ghana imemtimua Kocha Mkuu, Chris Hughton, baada ya Black Stars kutolewa katika hatua ya makundi kwenye michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCO), Shirikisho la Soka la Ghana ( GFA), limethibitisha.

Miamba hao wa Afrika Magharibi walichukua pointi mbili pekee kutoka kwenye mechi zao tatu za Kundi B, na matumaini ya kusonga mbele kama moja ya timu nne bora zilizo katika nafasi ya tatu yalizimwa Jumanne kwa ushindi wa kushtukiza wa Mauritania dhidi ya Algeria mjini Bouake.

> **"Chama cha Soka cha Ghana kinapenda kutangaza Chris Hughton ameondolewa kwenye majukumu yake kama kocha mkuu wa Timu ya Taifa ya wakubwa mara moja," ilisema taarifa ya GFA.**

"Chama cha Soka cha Ghana katika siku zijazo kitatoa ramani ya mwelekeo wa baadaye wa Black Stars."

Wasaizidi wa Hughton akiwamo kiungo wa zamani wa Aston Villa, George Boateng, kipa wa zamani wa Black Stars, Richard Kingston na Didi Dramani wote pia wameondolewa kwenye nafasi zao.

"Baraza la Utendaji pia limechukua uamuzi wa kuvunja timu ya ufundi ya Black Stars," ilimalizia taarifa hiyo.

Hughton mwenye umri wa miaka 65, kocha wa zamani wa Newcastle United na Brighton & Hove Albion, alichukua nafasi ya kuinoa Ghana kuanzia Februari, mwaka jana baada ya kuwa mshauri wa kiufundi wa shirikisho hilo kwa mwaka uliopita.

Alichukua nafasi hii wakati wa Kombe la Dunia la 2022, Ghana ilipotolewa katika hatua ya makundi, akichukua nafasi ya Otto Addo, mara baada ya michuano hiyo nchini Qatar.

Hata hivyo, Hughton, ambaye baba yake alikuwa ni Mghana, amesimamia kampeni ya kusikitisha ya Kombe la Mataifa ya Afrika kwa mabingwa hao mara nne.

Licha ya kuchukua uongozi, walifungwa 2-1 na vijana Cape Verde katika mchezo wao wa kwanza, wakiruhusu bao la dakika ya 92 kabla ya kutoka sare ya 2-2 na Misri katika mechi yao ya pili ya hatua ya makundi.

Ushindi waliohitaji kusonga mbele katika mchezo wao wa mwisho wa kundi dhidi ya Msumbiji ulikuwa tayari kushika kasi kufuatia mikwaju miwili ya Jordan Ayew, ambapo Mambas walisawazisha ka mabao mawili katika kipindi cha pili na kuokoa sare ya 2-2.

Hii iliiacha Ghana katika nafasi ya tatu kwa pointi mbili, na baada ya matokeo katika makundi mengine kwenda kinyume na wao, Black Stars walithibitishwa kuondolewa katika michuano hiyo siku ya Jumanne.

"Unaposhindwa kuona mchezo unaisha, inakuwa ngumu sana," alisema. "Maonyesho yetu hayakuwa mazuri.

"Tulicheza michezo mitatu, tukaruhusu mabao mawili katika kila mchezo na tuna hali ngumu.

"Tathmini yangu ya matokeo hayajakuwa mazuri vya kutosha."

# CAMEROON IMEJIFUNZA KWENYE MAKOSA - WOOH




**ABIDJAN,** Ivory Coast

MLINZI wa Cameroon, Christopher Wooh, amesema timu hiyo ilijifunza kutokana na makosa yao katika michezo iliyopita na kuyafanyia kazi hatimaye kupata ushindi wao wa mabao 3-2 dhidi ya Gambia kwenye mechi ya mwisho ya hatua ya makundi iliyochezwa juzi usiku, imeelezwa.

Wooh alifunga bao la ushindi kwa Simba Wasiofugika na kutinga hatua ya mtoano ya 16 Bora.

Akizungumza baada ya kupata ushindi huo, beki huyo alisema walichukua masomo muhimu katika michezo yao ya awali na kuamua kutokata tamaa hadi mchezo huo utakapomalizika.

"Tulijua hatupaswi kukata tamaa; ilitubidi kuthibitisha tulikuwa na nguvu ya kusonga mbele na tulijifunza kutokana na makosa yetu," alisema.

Cameroon sasa wamesonga mbele wakiwa na pointi nne na Wooh amesema hawafikirii kuhusu uchezaji wa mtu binafsi bali kile wanachotoa kwa pamoja.

"Ninafikiria kwa pamoja na lengo ni kushinda, tutashiriki mashindano haya na tutakuwa na michezo inayofuata na tunataka kupata matokeo mazuri," aliongeza.

# Seck apagawa bao la kwanza AFCON



**YOMOUSSOUKRO,** Ivory Coast

BEKI wa Senegal, Abdoulaye Seck, amesema ana furaha kuchaguliwa kuwa mchezaji bora wa mchezo baada ya kuchangia ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Guinea katika mechi ya mwisho ya Kundi C ya Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) iliyochezwa kwenye Uwanja wa Charles Konan Banny mjini Yamoussoukro, juzi usiku.

Beki huyo ambaye sio tu alisaidia kuweka bao safi, lakini pia alifunga bao kwa timu yake iliyowaongoza kumaliza kileleni katika kundi hilo.

"Namshukuru Mungu pamoja na wachezaji wenzangu ambao wote walichangia hili. Nilifunga bao langu la kwanza katika Kombe la Mataifa ya Afrika, na pia nina furaha nilichaguliwa kuwa mchezaji bora wa mechi," alisema mara baada ya mchezo huo.

"Tulijua mambo hayangekuwa rahisi. Tulishinda mechi zetu zote katika raundi ya kwanza. Sasa zimesalia mechi nne. Ni lazima tuweke miguu yetu chini na kuendelea kufanya kazi."

Beki huyo pia aligusia umuhimu wa uvumilivu sehemu yako katika timu.

"Siku zote huwa mvumilivu nisipocheza. Sikushiriki katika mechi yoyote wakati wa michuano iliyofanyika Cameroon.

"Nilikuwa mvumilivu na kuweka imani yangu kwa kocha na wachezaji wenzangu. Nilikuwa naiunga mkono timu na niliendelea kucheza kwa bidii huku nikitanguliza timu," alisema.

# 'Angola tunaishi kama familia'

**YOMOUSSOUKRO,** Ivory Coast

MLINZI wa Angola, Kialonda Gaspar, alifichua mafanikio ya kikosi chao yanatokana na ukweli wanachukuliana kama familia.

Hii ilikuwa ni baada ya beki huyo kuchaguliwa kuwa mchezaji bora wa mechi katika mchezo wao wa mwisho ya Kundi D iliyoshuhudia wakishinda 2-0 dhidi ya Burkina Faso, Jumanne.

Ushindi huo uliwawezesha kutinga hatua ya 16 bora ya Kombe la Mataifa ya Afrika katika mchezo huo uliopigwa kwenye Uwanja wa Charles Konan Bani, mjini hapa.

"Sisi katika timu ya taifa tunaishi kama familia moja na hilo ndilo linalotufanya tuwe imara uwanjani. Lengo langu linabaki kuisaidia timu ya taifa, na tuna uwezo wa kusonga mbele. Tutaendelea kujiandaa kwa shindano lililosalia," alisema Gaspar.

Akizungumzia mechi yao dhidi ya Burkina Faso, ambao pia wanasonga mbele kama washindi wa pili, beki huyo alisifu ufahamu wa mbinu wa timu yake dhidi ya timu hiyo.

"Tulikuwa wazuri uwanjani dhidi ya Burkina Faso. Vile vile huenda kwa kipengele cha mbinu. Tulicheza vizuri kama kikundi wakati wa mechi, na tulikuwa bora zaidi uwanjani. Nadhani ni muhimu kufuzu. Hii ni kwa ajili yetu na mamilioni ya Waangola walioko nyumbani," alibainisha.



HABARI MICHEZO

# Namungo yasaka mechi Dar

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Namungo FC, Mwinyi Zahera, ambaye timu yake imeweka kambi Dar es Salaa, amesema anahitaji kupata mechi mbalimbali za kirafiki ili kuwaimarisha wachezaji wake kabla ya Ligi Kuu Tanzania Bara kurejea baadaye mwezi huu.

Namungo kutoka Lindi, inafanya mazoezi yake kwenye Uwanja wa Bandari uliopo Temeke, jijini.

Akizungumza na Nipashe jana, Zahera, alisema anaamini watatumia kwa umakini muda uliopo kurekebisha mapungufu aliyoyabaini ili kurejea katika ligi wakiwa imara.

Zahera alisema anafahamu Ligi Kuu Tanzania Bara sasa ina ushindani mkubwa na utaongezeka kuingia katika duru la pili ambalo kila timu inahitaji kufikia malengo iliyojiwekea.

"Tumerejea mazoezini kufanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza katika mechi zilizopita, lakini pia muhimu kutengeneza muunganiko wa wachezaji waliosajiliwa dirisha dogo wale walikukuwepo awali.

Mashabiki wazidi kuwa pamoja nasi kwa sababu tunaamini tutafanya vizuri, kazi iliyoko mbele yetu ni kupambana katika kila mechi tutakayocheza," alisema Zahera.

Yanga ndio mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara na Azam FC ndio vinara wa ligi hiyo yenye timu 16.




# COASTAL UNION YAUSUSA UBINGWA LIGI KUU BARA

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kuwa katika nafasi ya sita kwenye msimamo, uongozi wa Coastal Union ya Tanga umeanika malengo yake matatu makubwa huku ikijiweka pembeni kwenye mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Tayari kikosi cha Coastal Union kimeanza rasmi mazoezi yake kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani, ulioko Tanga ili kujiweka imara na mechi za ligi kuu inayotarajiwa kuendelea tena hivi karibuni.

**Mabosi wa timu hiyo kongwe wamelitaka benchi la ufundi kuhakikisha wanafikia malengo ya klabu hiyo.**

Ofisa Habari wa Coastal Union, Abbas El-Sabri, alisema jana pamoja timu hiyo kutopata matokeo mazuri katika mechi za awali katika mzunguko wa kwanza, lakini ushindi waliopata kwenye michezo ya hivi karibuni imewafanya kutotoka katika malengo yao.

"Lengo letu la kwanza ni kumaliza katika moja kati ya nafasi nne za juu, pili ni kukata tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa msimu ujao na tatu ni kutwaa Kombe la FA, tunaweza kufanikiwa yote, mawili au moja kati ya hilo, lakini haya ndiyo malengo yetu," alisema El-Sabri.

Aliongeza ana uhakika wana uwezo wa kufikia malengo hayo kutokana na usajili bora waliofanya kipindi cha dirisha dogo na 'kiu' ya kufanya vizuri ya kila mchezaji waliyemwongeza kwenye kikosi chao.

Wachezaji wapya waliosajiliwa na Coastal Union kipindi cha dirisha dogo la usajili ni pamoja na Mganda David Ouna, Salim Aiyee kutoka Mbuni FC na Mkongomani Kasindi Paulin.

Mabingwa hao wa mwaka 1988 wana pointi 19 baada ya kucheza michezo 14, wakishinda mechi tano, sare nne na kupoteza michezo mitano huku kibindoni wakiwa na mabao 11 ya kufunga.




Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wasichana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls), wakijiandaa kuivaa Zambia katika mechi ya kwanza ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Dunia (U-17), itakayochezwa Februari 2, mwaka huu. **PICHA: TFF**

# *Simba, Yanga mapinduzi*

INATOKA UK. 24

muda wa wiki moja, tayari wamesharejea uwanjani na sasa Gamondi ameanza kuwapa mazoezi ya kuuchezea mpira, ufundi na mbinu mbalimbali.

"Wachezaji wetu walianza na programu ya ufukweni, hiyo imemalizika, sasa wamerejea uwanjani kupata mbinu za kiufundi, huku sasa ndipo tunapoandaa 'dozi' ili ligi ikianza, tuendeleze tulipoishia," alisema Kamwe.

Katika usajili wa dirisha dogo, Yanga imeongeza wachezaji wapya wa watatu ambao ni Joseph Guede (huru), Augustine Okrah kutoka Bechem FC ya Ghana na Shekhan Ibrahim wa JKU.

Naye Meneja wa Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, amesema kikosi chao kimerejea kwenye uwanja wa mazoezi ili kujiandaa michezo iliyopo mbele yao na malengo yao ni kupata matokeo chanya katika kila mechi watakayocheza.

Ahmed alisema Simba inajiimarisha kwa sababu inahitaji kuwapa furaha mashabiki wake kwa kupata matokeo chanya katika Ligi Kuu Tanzania Bara na mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast watakayocheza mapema mwezi ujao.

"Timu inaingia kambini kurekebisha makosa yaliyojitokeza katika mechi zote tulizocheza chini ya Kocha Mkuu, Abdelhak Benchikha, tunaenda kujinoa kwa kazi moja tu ya kurudisha heshima ya klabu, tunataka tuendelee kuogopwa na timu mbalimbali za Afrika," Ahmed alisema.

Aliongeza kila mchezaji wa Simba anatakiwa kupambana na kuonyesha ubora ili kujihakikishia namba sasa na hapo baadaye kwa sababu bado mchakato wa usajili unaendelea 'ndani kwa ndani.'

"Baada ya mapumziko mafupi, kikosi kimeanza rasmi mazoezi, mtaalamu wetu Benchikha amekuja kwa ari kubwa na kuhakikisha anaandaa kikosi imara na tishio.

Alisema mazunguko wa pili watakuja kivingine kwa sababu mipango ya benchi la ufundi ni kuona timu inatwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara na Kombe la FA, lakini ikicheza hatua ya nusu fainali ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu.

# Michezo

Alhamisi Januari 25, 2024

Nipashe



Ghana nje, yamtimua Hughton

UKURASA 21



Wachezaji wa Timu ya Taifa ya Cameroon wakishangilia baada ya timu yao kupata ushindi katika mechi ya Kundi C ya Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), dhidi ya Gambia iliyochezwa juzi usiku. Cameroon ilishinda mabao 3-2. **PICHA: MTANDAO**

# Simba, Yanga mapinduzi

## ●●● Vigogo hao wawataka nyota wake kubadilika licha ya dirisha la...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

WAKATI zikianza mawindo kwa ajili ya kuendelea na vita ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba na Yanga zimeweka wazi hazijamaliza 'panga' na kuachana na wachezaji ambao watabainika wameshuka viwango na hawawezi kuzisaidia timu hizo kufikia malengo, imefahamika.

**Simba na Yanga pia ziko katika hatua ya makundi ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, yatakayoendelea mapema mwezi ujao.**

Hata hivyo taarifa za ndani kutoka Yanga zinasema huenda mchezo huo wa kirafiki ukawa dhidi ya JKU kutoka Zanzibar.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema kocha wao (Migueal Gamondi), ameomba kupatiwa mechi za kirafiki ili kuwapima wachezaji wake wapya waliosajiliwa dirisha dogo lakini pia kuwaimarisha wakati wengine wako kwenye Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), ambao anaamini watarejea wakiwa 'moto'.

Kamwe alisema tayari viongozi wa timu hiyo wameshafanyia kazi maombi ya Gamondi, lakini akaongeza tarehe kamili na timu ambazo watacheza zitaamuliwa na Idara wa Ufundi.

Alisema pia licha ya dirisha dogo la usajili kufungwa, klabu itaendelea na mchakato wa usajili na 'kuwatema' nyota ambao watabainika wameshindwa kuonyesha ubora ambao mwalimu anauhitaji.

"Mazoezi yanaendelea vyema, tunatarajia kucheza mechi za kirafiki, tunasubiri ripoti kutoka idara yetu ya ufundi ambayo inafanya kazi kwa karibu na benchi la ufundi, wao watatuambia ni lini na aina gani ya timu wanayoihitaji kwa ajili ya mechi hiyo.

Najua muda mrefu umepita watu hawajaiona Yanga ikicheza, tunatarajia mechi hiyo itavutia watu wengi kwa sababu pia itatumika kuwanoa au kuwaangalia wachezaji wetu wapya tuliowasajili kipindi cha dirisha dogo," alisema Kamwe.

Aliongeza baada ya kumaliza mazoezi makali ya utimamu wa mwili ufukweni na gym waliyoyafanya kwa

INAENDELEA UK. 23

## Seck apagawa bao la kwanza AFCON

**YOMOUSSOUKRO,** Ivory Coast

BEKI wa Senegal, Abdoulaye Seck, amesema ana furaha kuchaguliwa kuwa mchezaji bora wa mchezo baada ya kuchangia ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Guinea...



HABARI UK. 22

## Coastal Union yaususa ubingwa Ligi Kuu Bara

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kuwa katika nafasi ya sita kwenye msimamo, uongozi wa Coastal Union ya Tanga umeanika malengo yake matatu makubwa...



HABARI UK. 23

## 'Angola tunaishi kama familia'

**YOMOUSSOUKRO,** Ivory Coast

MLINZI wa Angola, Kialonda Gaspar, alifichua mafanikio ya kikosi chao yanatokana na ukweli wanachukuliana kama familia...



HABARI UK. 22